



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA  
WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA  
ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2023**

**MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA  
WATAHINIWA KATIKA MTHANI WA KUMALIZA  
ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2023**

**MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI**

*Kimechapwa na:*  
Baraza la Mitihani la Tanzania,  
S.L.P. 2624,  
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI.....	iv
1.0 UTANGULIZI .....	1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI..	2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi .....	2
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi.....	46
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI .....	58
4.0 HITIMISHO .....	58
5.0 MAPENDEKEZO .....	59
Kiambatisho: Ulingafu wa Ufauluwa Watahiniwa Katika Kila Umahiri kwa Mwaka 2022 na 2023 .....	60

## **DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2023 katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, watunga sera na mitaala na wadau wengine wa elimu. Matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa na ujuzi ambao watahiniwa waliweza kupata au kutopata wakiwa shuleni.

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika, changamoto mbalimbali walizozionesha watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Pia, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa kila umahiri umebainishwa ili kuweza kubaini ni umahiri upi ulikuwa na changamoto zaidi miongoni mwa watahiniwa.

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa inaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa na ujuzi uliowawezesha kubaini matakwa ya maswali. Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama za chini walionesha kutokuwa na maarifa na ujuzi katika nyanja zilizotahiniwa na kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha. Kwa ujumla watahiniwa waliofanya vibaya walitoa majibu yasiyo sahihi na wengine hawakujibu baadhi ya maswali au walitoa jibu zaidi ya moja kwa swali la 1 – 40 kinyume na maelekezo ya mtihani.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zitapatiwa ufumbuzi ili kuongeza maarifa na ujuzi kwa watahiniwa wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohammed  
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ulifanyika tarehe 14 Septemba, 2023. Jumla ya watahiniwa 1,397,293 walisajiliwa kufanya mtihani huu ambapo watahiniwa 1,356,301 sawa na asilimia 97.06 walifanya mtihani na miongoni mwao watahiniwa 1,049,779 (77.40%) walifaulu.

Somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi lilikuwa na jumla ya maswali 45 yaliyogawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua jibu sahihi na sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali la 1 - 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu maalum ya kujibia (Optical Mark Reader – OMR). Katika kujibu swali la 41 - 45 watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi, upande wa nyuma wa karatasi maalum ya OMR.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi imewekwa alama ya nyota (\*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali wamewekwa katika uchambuzi na kupewa jina “Mengine”. Hii inamaanisha watahiniwa hao hawakujibu kabisa swali husika, au walichagua jibu zaidi ya moja kama inavyoonekana katika majedwali. Katika uchambuzi huu idadi ya watahiniwa na asilimia zao katika kila chaguo imeoneshwa. Ubora wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika kila swali unategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu au vipotoshi zimeainishwa.

Kigezo cha ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu kinategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi kama ifuatavyo: endapo asilimia 0 hadi 39 ya watahiniwa watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali utaelezwa kuwa ni hafifu.

Endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali utaelezwa kuwa mzuri endapo asilimia 60 ya watahiniwa au zaidi watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi.

Umahiri uliotahiniwa katika PSLE 2023 somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni *kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali swali la 1 - 9 na 44; kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku swali la 10 - 16 na 43; kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka swali la 17 - 25, 42 na 45; kutambua misingi ya uzalendo katika jamii swali la 26 - 35 na 41. kumudu mapishi mbalimbali swali la 36; kusanifu kazi za sanaa swali la 37; kutumia misingi ya unadhifu swali la 38 na 39 na Kutumia stadi za ujasiriamali swali la 40.*

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

**Swali la 1:** Kitendo cha kutekeleza wazo jipya kwa nia ya kuboresha bidhaa au huduma huitwaje?

- A Biashara      B Fursa      C Uwekezaji  
D Ubunifu      E Ujasiriamali

#### Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	199,999	101,481	131,327	602,556	305,008	15,930
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	14.75	7.48	9.68	44.43	22.49	1.17

Swali lilitathmini uwezo wa mtahiniwa kutambua ujuzi unaotumika kuboresha ubora wa bidhaa au huduma. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu watahiniwa 602,556 (44.43%) walichagua jibu sahihi *D, Ubunifu*. Watahiniwa hao

walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu ujasiriamali kwani walifahamu kuwa, ubunifu ni kitendo cha kutekeleza wazo jipya la kuboresha ubora wa bidhaa na huduma.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 606,488 (44.72%) walichagua vipotoshi *A, Biashara, B, Fursa* na *E, Mjasiriamali*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa, biashara ni mfumo wa kuuza na kununua bidhaa au huduma. Mjasiriamali ni mtu anayetumia rasilimali zinazomzunguka ili kujipatia kipato na fursa ni uwezo wa kutafsiri rasilimali zilizopo katika mazingira husika zinazoweza kumpa mtu faida. Kadhalika, watahiniwa 131,327 (9.68%) waliochagua kipotoshi *C, Uwekezaji* hawakutambua kuwa uwekezaji ni kitendo cha kutumia mtaji au amana aliyonayo mtu kwa lengo la kupata faida.

**Swali la 2:** Kazimoto ni mjasiriamali ambaye huisaidia jamii kutatua matatizo. Je, Kazimoto ni mjasiriamali wa aina gani?

- A Mfanyabiashara    B Mwelimishaji    C    D Kijamii  
E Mtumishi        wa F Mstahimilivu  
      umma

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	254,596	649,899	137,003	169,726	129,121	15,956
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	18.77	47.92	10.10	12.51	9.52	1.18

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha aina ya Mjasiriamali anayejishughulisha na kutatua matatizo ya jamii. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,203,342 (88.72%) walichagua vipotoshi *A, Mfanyabiashara, B, Mwelimishaji D, Mtumishi wa Umma* na *E, Mstahimilivu*. Watahiniwa 1,033,616 (76.21%.) waliochagua vipotoshi *A, Mfanyabiashara, B, Mwelimishaji* na *E, Mstahimilivu* hawakuelewa kuwa, mfanyabiashara ni mtu anayeuzua au kununua bidhaa na huduma kwa lengo la kupata faida. Mwelimishaji ni mtu anayeelimisha jamii lakini si mjasiriamali. Mstahimilivu ni mtu mwenye hulka ya kuwa



mvumilivu katika hali ngumu au kujikwamua haraka kutoka katika hali ngumu kitu ambacho hakihusiani na aina za ujasiriamali. Vivyo hivyo, watahiniwa, 169,726 (12.51%) waliochagua kipotoshi *D, Mtumishi wa Umma* hawakuwa na ufahamu wa kutosha kutambua kuwa mtumishi wa umma ni mfanyakazi aliyeajiriwa na serikali kwa lengo la kujiongezea kipato na sio kusaidia jamii.

Hata hivyo, watahiniwa 137,003 (10.10%) walichagua jibu sahihi *C, Kijamii* walikuwa na uelewa wa aina za wajasiriamali hivyo walibaini kuwa mjasiriamali jamii ni aina ya mjasiriamali anayeshughulika na kutatua matatizo ya jamii inayo mzunguka.

- Swali la 3:** Ipi **si** changamoto inayowakabili wajasiriamali wadogo wadogo nchini Tanzania?
- A Ukosefu wa malighafi
  - B Upungufu wa mtaji
  - C Mahitaji kidogo ya bidhaa
  - D Kutokuwa na soko la uhakika
  - E Kukosekana kwa urasimu

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	220,696	186,337	265,737	260,836	404,000	10,335
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	16.27	13.74	19.59	19.23	29.79	1.38

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha jambo ambalo siyo changamoto inayowakabili wajasiriamali wadogo wadogo nchini Tanzania. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa hafifu kwa sababu watahiniwa 933,606 (68.83%) walichagua vipotoshi *A, Ukosefu wa malighafi, B, Upungufu wa mtaji, C, Mahitaji kidogo ya bidhaa* na *D, Kutokuwa na soko la uhakika*. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mambo yanayoathiri maendeleo ya wajasiriamali wadogo wadogo nchini Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa ukosefu wa malighafi, upungufu wa mtaji, mahitaji



kutafuta malisho na maji. Ufugaji wa asili unahusisha mifugo kuzurura nje ikiwa huru kutafuta malisho na maji. Aidha, ufugaji wa mtu binafsi siyo aina ya ufugaji kwani mtu binafsi anaweza kujihusisha na aina yoyote ya ufugaji kama vile, ufugaji wa kuhamahama, ufugaji wa ndani, ufugaji katika ranchi na ufugaji wa asili.

- Swali la 5:** Wanafunzi wa Darasa la Sita wa shule ya msingi Mafanikio walipewa zawadi ya kutembelea hifadhi ya taifa ya Serengeti baada ya kufaulu vizuri mtihani wa mwisho wa mwaka. Je, hii ni aina gani ya utalii?
- A Utalii wa wanafunzi    B Utalii wa nje  
 C Utalii wa mapori        D Utalii wa hifadhi ya Taifa  
 E Utalii wa ndani

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	134,000	156,614	60,869	285,747	703,235	15,836
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	9.88	11.55	4.49	21.07	51.85	1.16

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha aina ya utalii unaofanywa na kikundi cha watu kinapotembelea eneo mojawapo ndani ya nchi yao. Kwa ujumla, ufaulu wa swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 703,235 (51.85%) walichagua jibu sahihi *E, Utalii wa ndani*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya aina za utalii kwani walijua kwamba, utalii wa ndani unahusisha kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine ndani ya nchi kwa ajili ya kupata burudani, biashara au kujifunza.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 637,230 (46.98%) walichagua vipotoshi A, B, C na D. Kipotoshi *A, Utalii wa wanafunzi* siyo aina ya utalii japokuwa wanafunzi hufanya ziara katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kujifunza. Kipotoshi *B, Utalii wa kimataifa* ni kitendo cha kusafiri kwenda nchi nyingine tofauti na unakoishi kwa ajili ya burudani, kujifunza, biashara au makusudi mengine.

Waliochagua vipotoshi *D, Utalii wa hifadhi ya Taifa* na *C, Utalii wa mapori* walishindwa kuelewa kuwa hizo siyo aina za utalii bali ni vivutio vya utalii na mapori ya akiba.

**Swali la 6:** Kipi kinasababisha kuongezeka kwa maji baharini yanayosababisha mmomonyoko wa fukwe na kuharibika kwa majengo yaliyopo pembezoni mwa bahari ya Hindi?

- A Kuyeyuka kwa theluji katika mlima Kilimanjaro
- B Kuyeyuka kwa theluji katika ncha za dunia
- C Kubadilika kwa misimu ya mwaka
- D Kuongezeka kwa ufugaji
- E Kuendesha shughuli za kilimo kwenye maeneo ya pwani

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	531,979	243,808	331,538	90,176	140,603	18,197
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	39.22	17.98	24.44	6.65	10.37	1.34

Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa kubainisha sababu kuu ya kuongezeka kwa kina cha bahari. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahinwa 1,094,296 (80.68%) walichagua vipotoshi *A, kuyeyuka kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro C, Mabadiliko ya misimu ya mwaka D, kuongezeka kwa ufugaji* na *E, kuendesha shughuli za kilimo katika ukanda wa pwani*. Watahiniwa 531,979 (39.22%) waliochagua kipotoshi *A, kuyeyuka kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro*, hawakuwa na uelewa kuwa ni kiasi kidogo sana cha barafu inayoyeyuka katika mlima Kilimanjaro na hivyo haiwezi kusababisha kuongezeka kwa kina cha Bahari.

Kwa upande mwingine watahiniwa wengine 331,538 (24.44%) waliochagua kipotoshi *C, Mabadiliko ya misimu ya mwaka*, walishindwa kuelewa kwamba, mabadiliko ya misimu ya mwaka ni matokeo ya dunia kulizunguka jua hivyo haina uhusiano wowote na

kuongezeka kwa kina cha bahari. Vilevile, kwa watahiniwa 230,779 (17.02%) waliochagua vipotoshi *D*, *kuongezeka kwa ufugaji na E*, *kuendesha shughuli za kilimo katika ukanda wa pwani*. Watahiniwa hao walishindwa kufahamu kuwa kuongezeka kwa kina cha maji baharini kunasababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, walikosa maarifa ya sababu na athari za mabadiliko ya tabia nchi duniani kwani vipotoshi vyote viwili havihusiani na sababu za kuongezeka kwa kina cha bahari. Kuongezeka kwa ufugaji ni matokeo ya ufugaji mzuri na wenye tija ambao unazingatia mazingira mazuri ya kufugia ambayo wanyama wanapata malisho ya kutosha, maji na huduma nzuri za afya. Aidha, kuendesha shughuli za kilimo maeneo ya pwani hairuhusiwi kwa sababu inachangia kusababisha mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa maeneo ya pwani.

Hata hivyo, watahiniwa 243,808 (17.98%) walichagua jibu sahihi *B*, *kuyeyuka kwa theluji katika ncha ya dunia*. Watahiniwa hao walielewa athari zinazosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Mabadiliko hayo yanasababisha kuyeyuka kwa barafu iliyopo katika ncha za dunia. Barafu hiyo inapoyeyuka husababisha kuongezeka kwa kina cha maji katika bahari.

**Swali la 7:** Chikichi ni zao mojawapo linalolimwa nchini Tanzania na hutumika kama malighafi ya kuzalishia mafuta ya mawese. Zao hili hulimwa katika mikoa ipi?

- A Kigoma, Tabora na Morogoro
- B Tabora, Kilimanjaro na Mara
- C Morogoro, Tabora na Mbeya
- D Dar es Salaam, Singida na Dodoma
- E Mara, Kagera na Geita

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	500,431	155,120	268,874	193,390	218,260	20,226
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	36.90	11.44	19.82	14.26	16.09	1.49

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mikoa inayolima zao la michikichi nchini Tanzania. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 835,644 (61.61%) walichagua vipotoshi *B, Tabora, Kilimanjaro na Mara C, Morogoro, Tabora na Mbeya D, Dar es Salaam, Singida na Dodoma na E, Mara, Kagera na Geita*. Watahiniwa 617,384 (45.52%) waliochagua vipotoshi *B, Tabora, Kilimanjaro na Singida C, Morogoro, Tabora na Mbeya na D, Dar es Salaam, Singida na Dodoma*, walishindwa kuelewa aina za mazao yanayolimwa katika mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa mkoa wa Kilimanjaro ni maarufu kwa kilimo cha zao la kahawa, Singida zao la Alizeti, Mbeya zao la Mpunga na Mahindi, Dodoma zao la Zabibu na Mara zao la Mtama. Watahiniwa wengine 218,260 (16.09%) waliochagua kipotoshi *E, Mara, Kagera na Geita*, hawakuelewa kuwa Kagera ni maarufu kwa kilimo cha zao la ndizi na kahawa ilhali Mara na Geita ni maarufu kwa kilimo cha Pamba.

Aidha, watahiniwa 500,431 (36.90%) walichagua jibu sahihi *A, Kigoma, Tabora na Morogoro*. Watahiniwa hao waliweza kutambua mikoa inayolima zao la michikichi nchini Tanzania kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya shughuli za kiuchumi nchini Tanzania hususan uzalishaji wa mazao.

**Swali la 8:** Mtaalamu wa kilimo aliwashauri wakulima wanaoishi maeneo yenye ukame kulima mazao yanayostahimili ukame. Mazao yapi unafikiri aliwashauri walime?

- A Mtama na uwele      B Mpunga na maharage  
 C Magimbi na viazi      D Mbogamboga na matunda  
 E Mahindi na ndizi

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	792,601	106,624	254,636	82,030	103,778	16,632
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	58.44	7.86	18.77	6.05	7.65	1.23

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini mazao yanayofaa kulimwa katika maeneo yenye ukame. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu watahiniwa 792,601 (58.44%) walichagua jibu sahihi *A, Mtama na Uwele*. Watahiniwa hao walifahamu kuwa, Mtama na Uwele hustahimili hali ngumu ya hewa kuliko nafaka nyinginezo. Pia walifahamu kuwa mazao haya hustawi katika eneo lenye mvua kidogo, udongo usio na rutuba nyingi na joto la kiwango cha juu.

Tofauti na hivyo, jumla ya watahiniwa 547,068 (40.34%) walichagua vipotoshi; *B, Mpunga na maharage, C, Viazi vikuu na viazi, D, Mbogamboga na matunda na E, Mahindi na ndizi*. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu namna ambavyo hali ya hewa huchangia kufanyika kwa shughuli fulani ya kiuchumi katika eneo husika. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kuwa, mpunga, viazi mbogamboga, matunda, mahindi na ndizi huhitaji mvua za kutosha kuanzia milimita 700 - 2500, udongo unaotunza unyevu na wenye rutuba na joto la wastani.

**Swali la 9 :** Ipi si changamoto inayokabili mbuga za wanyama nchini Tanzania ?

- A Kuongezeka kwa rasilimali fedha
- B Kuongezeka kwa vifaa vya kisasa vya mawasiliano
- C Kuongezeka kwa vyanzo vya maji na malisho
- D Kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyamapori na binadamu
- E Kuongezeka kwa uwindaji haramu

**Jedwali Na. 9: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	391,231	304,284	269,955	162,046	207,744	21,041
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	28.85	22.43	19.90	11.95	15.32	1.55

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini changamoto ambayo haizikabili mbuga za wanyama nchini Tanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika

swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,065,305 (78.54%) walichagua vipotoshi *A, Kuongezeka kwa rasilimali fedha B, Kuongezeka kwa vifaa vya kisasa vya mawasiliano D, Kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyama pori na binadamu na E, Kuongezeka kwa uwindaji haramu*. Watahiniwa 695,515 (51.28%) waliochagua vipotoshi *A, Kuongezeka kwa rasilimali fedha na B, Kuongezeka kwa vifaa vya kisasa vya mawasiliano*, hawakuwa na uelewa kwamba, ili kupata rasilimali fedha ni lazima kuboresha idara husika jambo ambalo si la muda mfupi. Pia, vifaa vya kisasa vya mawasiliano husababisha kukosekana kwa utulivu jambo linaloathiri hali ya asili ya kimazingira ambayo husababisha madhara kwa wanyama.

Vivyo hivyo, watahiniwa 369,790 (27.26%) walichagua vipotoshi *D, Kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyama pori na binadamu na E, Kuongezeka kwa uwindaji haramu*. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa kuwa, kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyamapori na binadamu inaongeza kesi za wanyamapori kuvamia makazi ya watu kitu kinachosababisha uharibifu wa mashamba au wanyama kuuwawa. Sambamba na hilo, kuongezeka kwa uwindaji haramu ni changamoto kwasababu, uwindaji haramu husababisha wanyama kuhama kwa lazima kwa hofu ya kuuwawa. Pia, uwindaji haramu husababisha wanyama kufa na kuisha kabisa ikiwa hatua madhubuti za kuzuia ujangili hazitachukuliwa.

Pamoja na watahiniwa wengi kushindwa kuchagua jibu sahihi, watahiniwa 269,955 (19.90%) walichagua jibu sahihi *C, kuongezeka kwa vyanzo vya maji na malisho*. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu kuhusu changamoto zinazokabili mbuga za wanyama nchini Tanzania na kuweza kubaini jambo ambalo siyo changamoto inayokabili mbuga za wanyama nchini Tanzania.



**Swali la 10:** Sikika alichora ramani ya mtaa wao bila kuonesha kipimio cha ramani. Unafikiri ni madhara gani atayapata mtumiaji wa ramani hiyo?

- A Kushindwa kufahamu mipaka ya mtaa
- B Kutozitambua alama zilizotumika
- C Kushindwa kuona maduka ya mtaani
- D Kutofahamu ukubwa halisi wa mtaa
- E Kushindwa kuona vizuri vitu mbalimbali

**Jedwali Na. 10: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	496,084	166,616	65,211	521,095	89,518	17,777
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	36.58	12.28	4.81	38.42	6.60	1.31

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini madhara atakayopata mtumiaji wa ramani ikiwa ramani itakosa kipimio cha ramani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani, watahiniwa 817,429 (60.27%) walichagua vipotoshi *A, Kushindwa kufahamu mipaka ya mtaa B, Kutozitambua alama zilizotumika C, Kushindwa kuona maduka ya mtaani na E, Kushindwa kuona vizuri vitu mbalimbali*. Watahiniwa 496,084 (36.58%) waliochagua kipotoshi *A, Kushindwa kufahamu mipaka ya mtaa*, hawakuwa na uelewa kuwa, mipaka huonyesha mwisho wa eneo na haitumiki katika kukokotoa ukubwa wa eneo. Vivyo hivyo, watahiniwa 231,827 (17.09%) waliochagua vipotoshi *B, Kutozitambua alama zilizotumika na C, Kushindwa kuona maduka ya mtaani*, hawakuwa na uelewa kuwa, hivyo ni vielelezo vinavyotumika kufafanua alama au rangi zilizotumika kwenye ramani. Pia, watahiniwa 89,518 (6.68%) waliochagua kipotoshi *E, Kushindwa kuona vizuri vitu mbalimbali*, walishindwa kuelewa kuwa kutokuona vitu mbalimbali katika ramani hakuna uhusiano wa moja kwa moja na uchoraji wa ramani na ukokotoaji wa eneo kwenye ramani.

Hata hivyo, watahiniwa 521,095 (38.42%) waliochagua jibu sahihi *D, Kutofahamu ukubwa halisi wa mtaa* walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya vipengele vya ramani hususani matumizi yake. Hivyo

waliweza kubaini kuwa bila kuwa na kipimio cha ramani ukubwa halisi wa eneo hautapatikana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ukubwa halisi wa eneo unapatikana kwa kukokotoa uwiano kati ya umbali ulioko katika ramani na umbali halisi kwenye ardhi.

**Swali la 11:** Ikiwa wanakijiji wa Yombo waliopo nyuzi 45 Mashariki huangalia habari kupitia TBC saa 2:00 usiku; ni muda gani Mtanzania aishiye Gambia nyuzi 30 Magharibi mwa Meridian Kuu ataangalia habari hiyo?

- A 1:00 jioni      B 1:00 asubuhi      C 3:00 usiku  
D 3:00 asubuhi      E 9:00 mchana

**Jedwali Na. 11: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	239,323	208,070	400,953	164,819	319,624	23,512
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	17.65	15.34	29.56	12.15	23.57	1.73

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini utofauti wa muda baina ya miji miwili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani, watahiniwa 1,013,165 (74.70%) walichagua vipotoshi A, 1:00 jioni, B, 1:00 asubuhi, D, 3:00 asubuhi na E, 9:00 mchana. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya matumizi ya mistari ya longitudo katika kutafuta muda wa mahali. Pia hawakuwa na uelewa kwamba, unapoelekea mashariki muda huongezeka na unapoelekea upande wa magharibi muda hupungua. Hata hivyo, baadhi yao walishindwa kutofautisha kati ya asubuhi na jioni. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi B, 1:00 asubuhi walishindwa kutofautisha asubuhi na jioni, wakati wengine walijumlisha masaa badala ya kutoa.

Vilevile watahiniwa 319,624 (23.57%) walichagua jibu sahihi E, 9:00 mchana. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya latitudo na longitudo hususan matumizi ya mistari ya longitudo katika kutafuta muda wa mahali. Watahiniwa hao walitafuta tofauti ya longitudo ya miji miwili ambayo ipo katika pande


mbili tofauti za Meridian Kuu yaani Mashariki na Magharibi na kujumlisha nyuzi za miji hiyo miwili ( $45^{\circ} + 30^{\circ} = 75^{\circ}$ ). Pia walitafuta tofauti ya muda kati ya Gambia na Yombo kama ifuatavyo.

$$\begin{aligned} \text{Saa } 1 &= 15^{\circ} \\ ? &= 75^{\circ} \\ \frac{75^{\circ} \times \text{saa } 1}{15^{\circ}} &= \text{saa } 5 \end{aligned}$$

Tofauti ya muda kati ya mji wa Gambia na Yombo ni masaa 5.

Watahiniwa hao walitambua kuwa unapoelekea mashariki muda unaongezeka na unapoelekea magharibi muda hupungua na kwa kuwa Gambia ipo Magharibi ya mji wa Yombo, ili kupata muda wa Gambia waliweza kutoa tofauti ya muda wa mji wa Yombo na muda wa mji wa Gambia (saa mbili usiku unatoa masaa matano unapata saa tisa mchana).

Watahiniwa wengine walibaini muda kwa kutumia chati/mchoro kama ifuatavyo.



Mchoro huu unawasilisha mistari ya longitude ambayo hutofautiana kwa nyuzi 15. Katika mistari hiyo, muda huongezeka kuelekea mashariki kutoka kwenye nyuzi 0 kwa saa moja kwa kila nyuzi 15, pia hupungua kwa saa moja kuelekea Magharibi. Hivyo kwa kutumia mistari hii watahiniwa waliweza kuandika kwa usahihi utofauti wa muda baina ya miji husika.

- Swali la 12:** Mwalimu Chapakazi aliwauliza wanafunzi, “Nini hutokea katika eneo la Ikweta wakati wa jua la utosi tarehe 21 Machi na tarehe 23 Septemba?” Jibu gani sahihi lilitolewa na mwanafunzi?
- A Usawa wa urefu wa mchana na usiku
  - B Mchana kuwa mrefu kuliko usiku
  - C Kutokea kwa giza na mwanga katika dunia
  - D Utofauti wa urefu wa mchana na usiku
  - E Usiku kuwa mrefu kuliko mchana

**Jedwali Na. 12: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	309,629	331,133	221,503	227,421	245,034	21,581
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	22.83	24.41	16.33	16.77	18.07	1.59

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini nini hutokea ukanda wa Ikweta jua linapokuwa la utosi tarehe 21 Machi na tarehe 23 Septemba. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,025,079 (75.58%) walichagua vipotoshi; *B, Mchana kuwa mrefu kuliko usiku, C, Kutokea kwa giza na mwanga katika dunia, D, Utofauti wa urefu wa mchana na usiku na E, Usiku kuwa mrefu kuliko mchana.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matokeo ya Dunia kulizunguka Jua. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, mchana kuwa mrefu kuliko usiku ni matokeo ya Dunia kuelekea Jua kwa upande wa ncha ya Kaskazini, kati ya tarehe 21 Machi na 23 Septemba. Kutokea kwa giza na mwanga katika dunia, ni matokeo ya kupatwa kwa Jua ambapo hutokea wakati mwezi unapokuwa katikati ya dunia na jua. Utofauti wa urefu wa mchana na usiku, ni matokeo ya dunia kulizunguka jua na usiku kuwa mrefu kuliko mchana, ni matokeo ya dunia kuelekea jua kwa upande wa ncha ya Kusini, kati ya tarehe 21 Machi na 23 Septemba.

Hata hivyo, watahiniwa 309,629 (22.83%) walichagua jibu sahihi A, *Usawa wa urefu wa mchana na usiku.* Uchaguzi wa jibu hili

unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya dunia kulizunguka jua na matokeo yake.

**Swali la 13:** Wataalamu wa anga huainisha anga hewa kulingana na mpangilio wake. Je, mpangilio upi ni sahihi?

- A Angatropo, Angastrato, Angameso na Angajoto
- B Angameso, Angastrato, Angajoto na Angatropo
- C Angastrato, Angameso, Angatropo na Angajoto
- D Angastrato, Angameso, Angatropo na Angajoto
- E Angastrato, Angatropo, Angameso na Angajoto

**Jedwali Na. 13: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	416,538	202,336	233,071	163,870	317,625	22,861
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	30.71	14.92	17.18	12.08	23.42	1.69

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kubaini mpangilio sahihi wa Angahewa. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa hafifu kwa sababu watahiniwa 916,902 (67.60%) walichagua vipotoshi; *B, Angameso, Angastrato, Angajoto na Angatropo, C, Angastrato, Angameso, Angatropo na Angajoto, D, Angastrato, Angameso, Angatropo na Angajoto* na *E, Angastrato, Angatropo, Angameso na Angajoto*. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi hivi kutokana na uelewa mdogo kuhusu Angahewa na matabaka yake kwani, majibu hayo hayakuwa na mpangilio sahihi. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, katika kipotoshi B, mpangilio umeanza na Angameso ambalo ni tabaka la angahewa la tatu kutoka katika uso wa dunia kuelekea angani linalopatikana juu ya Angastrato au kati ya Angastrato na Angajoto. Angajoto ni tabaka la angahewa la juu zaidi kutoka katika uso wa dunia linalopatikana juu ya mpaka wa Angameso. Vivyo hivyo, Angatropo ni tabaka la angahewa la chini au la kwanza kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani.

Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi; C, D na E, walishindwa kubaini kuwa, katika kipotoshi C, Angastrato ni tabaka la pili,

Angameso la tatu na Angatropo la kwanza. Katika kipotoshi D, Angastrato ni tabaka la pili, Angatropo la kwanza, Angajoto la nne na Angameso la tatu wakati katika kipotoshi E, Angastrato ni tabaka la pili na Angatropo la kwanza kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani.

Aidha, watahiniwa 416,538 (30.71%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Angatropo, Angastrato, Angameso na Angajoto*. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Angahewa na mpangilio sahihi wa matabaka yake.

**Swali la 14:** Mwanafunzi wa Darasa la Sita alichora mchoro wa jua, mwezi na tufe mtawalia katika mstari mnyoofu. Je, tukio lipi la kijiografia linawakilishwa na mpangilio wa mchoro hiyo?

- A Kupatwa kwa jua      B Kupatwa kwa mwezi  
 C Mfumo wa jua      D Mpangilio wa Sayari  
 E Usiku na mchana

**Jedwali Na. 14: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	423,894	349,,225	219,223	157,094	185,658	21,207
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	31.25	25.75	16.16	11.58	13.69	1.56

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha tukio la Kijiografia linalowakilishwa na mpangilio wa mchoro wa jua, mwezi na tufe mtawalia katika mstari mnyoofu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 911,200 (67.18%) walichagua vipotoshi; *B, Kupatwa kwa mwezi; C. Mfumo wa jua; D, Mpangilio wa Sayari na E, Usiku na mchana*. Uchaguzi huo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa Jua, dhana ya dunia kulizunguka Jua na matokeo yake. Kupatwa kwa mwezi ni tukio la Kijiografia linalowakilishwa na mpangilio wa mchoro wa jua, dunia na mwezi katika mstari mnyoofu. Mfumo wa jua ni mpangilio wa sayari nane na magimba mengine

yaliyoko angani kulizunguka jua. Mpangilio wa sayari ni namna ambavyo sayari zimejipanga katika umbali wa kutoka jua wakati mchana na usiku ni matokeo ya dunia kujizungusha kwenye mhimili wake.

Pamoja na watahiniwa wengi kushindwa kuchagua jibu sahihi, watahiniwa 423,894 (31.25%) walichagua jibu sahihi A, *Kupatwa kwa jua*. Uchaguzi wa jibu hili unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa Jua na matokeo ya dunia kulizunguka jua. Walielewa kuwa mpangilio wa jua, mwezi na tufe (dunia) husababisha kupatwa kwa jua.

**Swali la 15:** Wanafunzi watano wa Darasa la Nne walikuwa wanashindana kuchora mfumo wa jua. Yupi alipanga sayari kwa usahihi kutoka kwenye jua?

- A Zuhura, Dunia, Mirihi na Zebaki
- B Zebaki, Zuhura, Mirihi na Dunia
- C Zebaki, Zuhura, Dunia na Mirihi
- D Zebaki, Dunia, Zuhura na Mirihi
- E Dunia, Zuhura, Mirihi na Zebaki

**Jedwali Na. 15: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	96,090	147,331	894,224	79,825	128,059	10,772
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	7.08	10.86	65.93	5.89	9.44	0.79

Katika Swali hili mtahiniwa alitakiwa kubaini mpangilio sahihi wa sayari katika mfumo wa jua. Ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 894,224(65.93%) walichagua jibu sahihi C, *Zebaki, Zuhura, Dunia na Mihiri*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu kuhusu mfumo wa jua na mpangilio sahihi wa sayari kutoka katika jua.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 451,305(33.27%), waliochagua vipotoshi A, *Zuhura, Dunia, Mirihi na Zebaki, B, Zebaki,*

Zuhura, Mirihi na Dunia, D, Zebaki, Dunia, Zuhura na Mihiri na E, Dunia, Zuhura, Mirihi na Zebaki, hawakutambua mpangilio sahihi wa sayari katika mfumo wa jua. Watahiniwa hawa walitakiwa kuelewa kuwa mpangilio wa sayari umefuata umbali wa sayari ilipo kutoka kwenye jua kwa mfuatano. Mpangilio uliopo kwenye vipotoshi haukuzingatia hilo. Kwa mfano, mpangilio katika kipotoshi A umeanza na Zuhura, ambayo ni sayari ya pili kutoka katika jua. Vile vile, kipotoshi E kimeanza na Dunia ambayo ni sayari ya tatu kwa umbali kutoka kwenye jua. Kipotoshi B hakikuwa sahihi kwa kuwa Mirihi sio sayari ya tatu kutoka kwenye jua na Dunia siyo sayari ya nne kutoka kwenye jua au katika mfumo wa jua bali ni ya tatu.

**Swali la 16:** Ikiwa umepewa nafasi ya kueleza kwanini mwezi hauwezi kutengeneza nishati ya umeme, ni sababu ipi ungeitoa?

- A Mwezi unaakisi mwanga wa jua
- B Mwezi unasharabu mwanga wa jua
- C Mwezi ni mdogo kuliko jua
- D Mwezi hutoa mwanga usiku tu
- E Mwezi hulizunguka jua

**Jedwali Na. 16: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	439,213	263,968	129,171	406,624	103,543	13,782
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	32.38	19.46	9.52	29.98	7.63	1.02

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa sababu ya kwanini mwezi hauwezi kutengeneza nishati ya umeme. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 670,592 (49.44%) waliochagua vipotoshi B, *Mwezi unasharabu mwanga wa jua* na D, *Mwezi hutoa mwanga usiku tu* walishindwa kuelewa kuwa, mwezi hautengenezi mwanga wake wenyewe, bali husharabu mwanga wa jua na kuakisi mwanga wa jua wakati wa giza. Vilevile, watahiniwa 129,171 (9.52%) waliochagua kipotoshi C, *Mwezi ni mdogo kuliko jua*, hawakutambua kuwa, udogo wa mwezi hauwezi kuwa sababu ya



kushindwa kutengeneza nishati ya umeme bali ni kutokuwa na mwanga wake wenyewe. Watahiniwa wengine 103,543 (7.63%) waliochagua kipotoshi *E*, *Mwezi hulizunguka jua* hawakutambua kuwa mwezi huizunguka sayari Dunia na siyo jua.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 439,213 (32.38%) walichagua jibu sahihi *A*, *Mwezi unaakisi mwanga wa jua*. Watahiniwa hao walitambua kuwa, mwezi hauna nishati ya umeme, bali unaakisi mwanga wa jua wakati wa usiku. Hivyo, nuru ya mwanga ulio akisiwa na mwezi haina nguvu inayo weza kutumika kuzalisha umeme.

**Swali la 17:** Iwapo jotoridi la Mji wa Dar es Salaam uliopo usawa wa bahari ni nyuzijoto za sentigredi 39, Je, Jotoridi la Mji wa Moshi uliopo mita 5000 kutoka usawa wa bahari litakuwa nyuzi ngapi?

- A 9°C                      B 39°C                      C 0°C  
D 69°C                      E 30°C

**Jedwali Na. 17: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	250,526	231,421	282,193	275,128	292,009	25,024
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	18.47	17.06	20.80	20.29	21.53	1.85

Swali lilimtaka mtahiniwa kutafuta tofauti ya joto baina ya mji wa Moshi na Jiji la Dar es salaam. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,080,751 (79.68%) walishindwa kuchagua jibu sahihi. Watahiniwa 292,009 (21.53%) waliochagua kipotoshi *E*, 30°C, walishindwa kuelewa kuwa ili kupata halijoto ya mji wa Moshi ulioko kwenye mwinuko zaidi ya mji wa Dar es Salaam walipaswa kutoa halijoto ya mji wa Moshi kutoka kwenye ile ya mji wa Dar es salaam. Vivyo hivyo, watahiniwa 506,549 (37.35%) waliochagua vipotoshi *B*, 39°C, na *D*, 69°C, hawakuwa na ufahamu kuhusu mambo yanayoathiri halijoto hasa mwinuko kutoka usawa wa bahari. Pia walikosa ujuzi wa kukokotoa mabadiliko ya joto kutokana na kuongezeka kwa mwinuko toka usawa wa bahari kati

ya mji mmoja na mwingine. Vilevile, watahiniwa 282,193 (20.81%) waliochagua kipotoshi C, 0°C hawakuwa na ufahamu kuwa, 0°C ni joto la usawa wa bahari. Swali lilitaka kutafuta joto la mji wa Moshi uliopo mita 5000 juu ya usawa wa bahari.

Kwa upande mwingine watahiniwa 250,526 (18.47%) walichagua jibu sahihi A, 9°C. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa na ujuzi wa kubaini kuwa, mabadiliko ya halijoto hutokana na ongezeko la mwinuko. Ni ukweli kuwa jotoridi hupungua kwa kiwango cha 0.6°C kwa kila ongezeko la mita 100 kutoka usawa wa bahari. Hivyo, watahiniwa walitumia kanuni sahihi kutafuta tofauti ya joto kati ya miji miwili kama ifuatavyo;

$$100 \text{ m} = 0.6^{\circ}\text{C}$$

$$5000 \text{ m} = X$$

$$x = \frac{5000\text{m} \times 0.6^{\circ}\text{c}}{100\text{m}} = 30^{\circ}\text{c}.$$

$$\therefore 39^{\circ}\text{c} - 30^{\circ}\text{c} = 9^{\circ}\text{c}$$

Walitoa 30°C kutoka 39°C kwa sababu halijoto inapungua kutoka usawa wa bahari na kupata joto la mji wa Moshi kuwa 9°C.

**Swali la 18:** Utatoa ushauri upi kwa watu waishio eneo la wazi na lenye upepo mkali?

- A Kuhama eneo hilo
- B Kujenga maghorofa
- C Kupanda miti
- D Kujenga nyumba zisizo za kudumu
- E Kujenga uzio kuzunguka eneo

**Jedwali Na. 18: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	182,454	62,174	962,213	54,039	82,535	12,886
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	13.45	4.58	70.94	3.98	6.09	0.96

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kubainisha ushauri atakaoutoa kwa watu wanaoishi katika eneo la wazi na lenye upepo mwingi. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 962,213 (70.94%) walichagua jibu sahihi *C, Kupanda miti*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utunzaji wa mazingira na walitambua njia mbalimbali za kutunza mazingira ikiwemo kupanda miti. Kupanda miti katika eneo lililo wazi na lenye upepo mwingi husaidia kuepusha ardhi kukumbwa na mmomonyoko wa udongo pamoja na kurejesha mbolea katika udongo. Mbali na hayo miti husaidia kuhifadhi unyevu katika udongo na kupunguza kasi ya upepo inayoweza kuharibu udongo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 182,454 (13.45%) waliochagua kipotoshi *A, Kuhama eneo hilo* hawakutambua kwamba kuhama siyo suluhisho la kutunza mazingira ya eneo lililo wazi na lenye upepo mkali. Watahiniwa wengine 198,748 (14.65%) walichagua vipotoshi *B, Kujenga maghorofa, D, Kujenga nyumba zisizo za kudumu* na *E, Kujenga uzio kuzunguka eneo*. Watahiniwa hao, walishindwa kutambua kuwa, hizi siyo njia sahihi za kutunza mazingira ya eneo lililowazi na lenye upepo mkali.

**Swali la 19:** Chautundu alichukua kipimajoto kutoka katika boksi la Stevenson na kukiweka sehemu ya wazi kwa saa nne. Baada ya muda, alisoma kiwango cha juu na chini cha jotoridi kama nyuzi 38°C na 26°C mtawalia. Upi ni utofauti wa kiwango cha jotoridi kwa siku hiyo?  
 A 12°C                      B 22°C                      C 26°C  
 D 38°C                      E 6°C

**Jedwali Na. 19: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	880,621	137,060	117,621	104,162	100,570	16,267
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	64.93	10.11	8.67	7.68	7.42	1.20

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini tofauti ya kiwango cha jotoridi kwa siku. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 880,621 (64.93%) walichagua jibu sahihi A, 12<sup>o</sup>C. Watahiniwa hao walifahamu kanuni ya kutafuta tofauti ya jotoridi kuwa ni kuchukua kiwango kikubwa cha jotoridi, kutoa kiwango kidogo cha jotoridi. Hivyo waliweza kutoa 38<sup>o</sup>C – 26<sup>o</sup>C = 12<sup>o</sup>C.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 237,630 (17.52%) waliochagua vipotoshi B, 22<sup>o</sup>C na E, 6<sup>o</sup>C walishindwa kutambua kanuni ya kutafuta utofauti wa kiwango cha jotoridi. Hivyo, walichagua majibu ambayo si sahihi. Vilevile, jumla ya watahiniwa 221,783 (16.35%) waliochagua vipotoshi C, 26<sup>o</sup>C na D, 38<sup>o</sup>C hawakuwa na uelewa wa namna ya kutafuta utofauti wa jotoridi. Kinyume na hapo, walichagua kiwango cha chini na kiwango cha juu cha jotoridi kama vilivyotolewa kwenye swali na kujaza kama jibu sahihi bila kukokotoa ili wapate tofauti yake.

**Swali la 20:** Tanzania imekwishaongozwa na Mawaziri Wakuu wengi tangu uhuru. Yupi alikuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

- A Rashid Mfaume Kawawa
- B Edward Moringe Sokoine
- C Cleopa Msuya
- D John Malechela
- E Edward Lowasa

**Jedwali Na. 20: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	627,031	457,847	80,646	64,670	110,212	15,895
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	46.23	33.76	5.95	4.77	8.13	1.16

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini Waziri Mkuu wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 627,031(46.23%) walichagua jibu sahihi A, *Rashid Mfaume Kawawa*. Watahiniwa hao walidhihirisha

kuwa na uelewa wa kutosha juu ya Mawaziri Wakuu mbalimbali waliotumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, waliweza kumtambua Waziri Mkuu wa kwanza aliyehudumu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1962 hadi 1977 wakati wa hatamu ya Mwalimu Julius K. Nyerere.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 457,847 (33.76%) waliochagua kipotoshi *B*, *Edward Moringe Sokoine*, hawakuelewa kuwa, yeye alihudumu kama Waziri Mkuu wa tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 hadi 1984. Vilevile, watahiniwa 80,646 (5.95%) walichagua kipotoshi *C*, *Cleopa David Msuya*, hawakuelewa kuwa, yeye alihudumu kama Waziri Mkuu wa nne mwaka 1980 hadi 1983 na pia 1994 hadi 1995. Vivyo hivyo, watahiniwa 64,670 (4.77%) waliochagua kipotoshi *D*, *John Malecela*, hawakuelewa kuwa, yeye alihudumu kama Waziri Mkuu wa Saba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1990 hadi 1994. Watahiniwa 110,212 (8.13%) waliochagua kipotoshi *E*, *Edward Lowasa*, hawakuelewa kuwa, yeye alikuwa Waziri Mkuu wa tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyehudumu kuanzia mwaka 2005 hadi 2008.

**Swali la 21:** Kwa nini Tanzania inatambulika kama chimbuko la binadamu?

- A Maeneo mengi ya kihistoria yanapatikana Tanzania.
- B Bustani ya Edeni inapatikana Tanzania.
- C Eneo kubwa la Tanzania lina misitu.
- D Dkt. L. Leakey na Dkt. M. Leakey walifanya utafiti wao Tanzania.
- E Mabaki ya binadamu wa kale yaligunduliwa Tanzania.

**Jedwali Na. 21: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	439,899	63,470	79,016	182,640	573,147	18,129
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	32.43	4.68	5.83	13.47	42.26	1.33

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua sababu ya Tanzania kutambulika kama chimbuko la binadamu. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 573,147 (42.26%) waliochagua jibu sahihi *E, Mabaki ya binadamu wa kale yaligunduliwa Tanzania*, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu chimbuko la binadamu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 182,640 (13.47%) waliochagua kipotoshi *D, Dkt. L. Leakey na Dkt. M. Leakey walifanya utafiti wao Tanzania*, hawakuelewa kuwa, hao walikuwa ni watafiti waliogundua fuvu la binadamu wa kale mwaka 1959 maeneo ya Olduvai Gorge. Fuvu hilo ndilo linalosababisha Tanzania kutambulika kama chimbuko la binadamu. Vilevile, watahiniwa 439,899 (32.43%) waliochagua kipotoshi; *A, Maeneo mengi ya kihistoria yanapatikana Tanzania*, hawakuelewa kuwa, pia, katika nchi zingine duniani kuna maeneo mengi ya kihistoria, lakini hiyo haiifanyi sehemu kuwa chimbuko la mwanadamu. Kwa kuongezea, watahiniwa 63,470 (4.68%) waliochagua kipotoshi *B, Bustani ya Edeni inapatikana Tanzania*, hawakuwa na maarifa kuwa, bustani ya Edeni haipatikani Tanzania. Watahiniwa wengine, 79,016 (5.83%) waliochagua kipotoshi *C, Eneo kubwa la Tanzania lina misitu*, hawakuwa sahihi, kwa sababu, kuwepo kwa misitu mingi hakuna uhusiano wowote na chimbuko la binadamu.

**Swali la 22:** Ni kwa sababu gani Mwalimu Julius K. Nyerere anajulikana kama “Baba wa Taifa”?

- A Alikuwa mwalimu
- B Alijitolea kuhamasisha kudai uhuru
- C Alihudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa
- D Aliongoza usuluhishi wa mgogoro wa Burundi
- E Aliongoza Tanganyika baada ya uhuru

**Jedwali Na. 22: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	92,538	878,178	79,992	49,690	241,914	13,989
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	6.82	64.75	5.90	3.66	17.84	1.03

Watahiniwa walitakiwa kutambua sababu ya kwanini Mwl Julius K. Nyerere hutambuliwa kama “Baba wa Taifa”. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo watahiniwa 878,178 (64.75%) walichagua jibu sahihi *B, Alijitolea kuhamasisha uhuru*. Uchaguzi wa jibu hili unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mchango wa Mwl.Nyerere katika ustawi wa Taifa la Tanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 92,538 (6.82%) waliochagua kipotoshi *A, Alikuwa mwalimu*, walidhihirisha kuwa na uelewa mdogo wa kutambua mchango wa Mwalimu katika Taifa hili. Ingawa, Mwl Julius K. Nyerere alikuwa mwalimu katika shule ya St. Mary’s (Shule ya Sekondari Milambo) na St. Fransis (Shule ya Sekondari Pugu) halikuwa jibu sahihi kwa sababu, wapo walimu wengi nchini, lakini, hawatambuliki kama Baba wa Taifa. Hivyo, kuwa mwalimu hakumfanyi mtu kuwa Baba wa Taifa. Hata hivyo, watahiniwa 79,992 (5.90%) waliochagua kipotoshi *C, Alihudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa*, walionesha uelewa hafifu juu ya kuwaenzi mashujaa wetu. Japokuwa, Mwl Julius K. Nyerere alienda Umoja wa Mataifa mwezi Machi 1955 hili halikidhi kumpa hadhi ya kuitwa Baba wa Taifa.

Vilevile, watahiniwa 49,690 (3.66%) waliochagua kipotoshi *D, Aliongoza usuluhishi wa mgogoro wa Burundi*, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mchango wa Mwl. Nyerere katika nchi ya Tanzania. Mwl. Nyerere alisuluhisha mgogoro wa Burundi baada ya kuwa ameshapata hadhi ya kuwa “Baba wa Taifa”. Watahiniwa wengine 241,914 (17.84%) waliochagua kipotoshi *E, Aliongoza Tanganyika baada ya uhuru*, inaonyesha uelewa mdogo walionao kuhusu Mwl Julius K. Nyerere. Ni kweli kuwa, Mwalimu Julius Nyerere alikuwa Rais wa kwanza baada ya uhuru, lakini, hii haitoshi

kumpa hadhi ya Baba wa Taifa. Hadhi ya kuwa kuwa “Baba wa Taifa” imetolewa ili kuenzi harakati alizoongoza za mapambano ya kuanzisha Taifa huru la Tanzania.

**Swali la 23:** Maeneo ya kihistoria hutunza aina tofauti ya habari za kihistoria kama vile michoro ya zamani, mabaki ya zana za kivita, majengo ya kale na maendeleo ya biashara. Aina gani ya habari za kihistoria hupatikana Isimila mkoani Iringa?

- A Masalia ya majengo ya biashara ya utumwa
- B Masalia ya utamaduni wa Kiarabu
- C Ustaarabu wa kale katika Tanganyika
- D Vita za kikoloni katika Tanganyika
- E Masalia ya Zana za Mawe za Kale

**Jedwali Na. 23: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	229,788	86,621	88,781	88,659	843,598	18,854
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	16.94	6.39	6.55	6.54	62.20	1.38

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini aina ya kumbukumbu ya kihistoria inayopatikana Isimila mkoani Iringa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 843,598 (62.20%) walioweza kuchagua jibu sahihi *E, Masalia ya Zana za Mawe za Kale*, walikuwa na maarifa yakutosha kuhusu maeneo ya kihistoria nchini Tanzania na kumbukumbu zake za kihistoria.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 229,788 (16.94%) walichagua kipotoshi *A, Masalia ya majengo ya biashara ya utumwa*. Watahiniwa hao walikosa maarifa ya maeneo ya kihistoria, hivyo, kushindwa kutambua kuwa, masalia haya hupatikana katika miji iliyopo pembezoni mwa bahari ya Hindi kama vile mji wa Bagamoyo mkoani Pwani. Baadhi ya watahiniwa 86,621 (6.39%) waliochagua kipotoshi *B, Masalia ya utamaduni wa Kiarabu* hawakufahamu kuwa



masalia ya utamaduni wa Kiarabu hupatikana katika miji iliyopo ukanda wa Pwani kama Kaole, Kilwa na Zanzibar. Vilevile, watahiniwa 88,781 (6.55%) waliochagua kipotoshi C, *Ustaarabu wa kale katika Tanganyika*, hawakuelewa kuwa, ustaraabu huo ulienea maeneo ya Pwani ya bahari ya Hindi.

Watahiniwa wengine 88,659 (6.54%) waliochagua kipotoshi D, *Vita za kikoloni katika Tanganyika*, walishindwa kuhusianisha eneo la kihistoria la Isimila na taarifa zinazohifadhiwa katika eneo hilo. Vita vya kupinga ukoloni vilipiganwa katika maeneo tofauti tofauti ya nchi kwa mfano; Lugalo, Kalenga, Songea, Kilwa, Mahenge, Tanga, Nyangao na Masasi. Uchaguzi wa vipotoshi unathibitisha uelewa hafifu wa watahiniwa juu ya maeneo ya kihistoria na taarifa zinazohifadhiwa.

- Swali la 24:** Ni madhara gani hutokana na uvuvi wa kutumia baruti na kokoro?
- A Uharibifu wa samaki na mazalia yake
  - B Mvuvi kutumia muda mrefu kupata samaki
  - C Wavuvi kutozwa kodi kubwa ya uvuvi
  - D Uharibifu wa vyombo vya usafirishaji majini
  - E Uwepo wa samaki wengi viwandani

**Jedwali Na. 24: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	1,037,435	79,500	66,102	105,682	54,544	13,038
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	76.49	5.86	4.87	7.79	4.02	0.97

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha athari za kutumia njia haramu za uvuvi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 1,037,435 (76.46%) walichagua jibu sahihi A, *Uharibifu wa samaki na mazalia yake*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu athari zinazotokana na uvuvi wa kutumia njia haramu, hususani, baruti na kokoro.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 305,828 (22.55%) walichagua vipotoshi; *B, Mvuvi kutumia muda mrefu kupata samaki, C, Wavuvi kutozwa kodi kubwa ya uvuvi, D, Uharibifu wa vyombo vya usafirishaji majini na E, Uwepo wa samaki wengi viwandani.* Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za uvuvi na madhara yake. Walishindwa kuelewa kuwa, kipotoshi B, ni athari ya kutumia zana duni za uvuvi ambazo hupelekea kupata kiasi kidogo cha samaki. Kipotoshi C na D, ni mikakati ya kudhibiti uvuvi haramu, na kipotoshi E, ni kikwazo cha maendeleo ya sekta ya uvuvi kutokana na mlundikano wa samaki viwandani.

**Swali la 25:** Seti ipi inawakilisha mambo yanayoathiri tabianchi ya eneo fulani katika uso wa dunia?

- A Gridi, Meridiani Kuu na sura ya nchi
- B Mstarihi, sura ya nchi na longitudo
- C Latitudo, mwinuko kutoka usawa wa bahari na sura ya nchi
- D Meridiani Kuu, mwinuko kutoka usawa wa bahari na longitudo
- E Sura ya nchi, longitudo na latitudo

**Jedwali Na. 25: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	173,829	120,965	604,950	249,773	189,162	17,622
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	12.82	8.92	44.60	18.42	13.95	1.30

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini seti ambayo inawakilisha mambo yanayoathiri tabianchi ya eneo fulani katika uso wa dunia. Ufaulu wa jumla ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 604,950 (44.60%) waliweza kuchagua jibu sahihi *C, Latitudo, mwinuko kutoka usawa wa bahari na sura ya nchi.* Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri kuhusu dhana ya tabianchi na mambo yanayoathiri tabianchi katika maeneo yote ya uso wa dunia. Walifahamu kuwa latitudo, mwinuko kutoka usawa wa bahari na sura ya nchi vinaathiri tabianchi ya eneo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 733,729 (54.10%) walichagua vipotoshi; *A, Gridi, Meridian Kuu na sura ya nchi, B, Mstarihi, sura ya nchi na longitudo, D, Meridiani Kuu, mwinuko kutoka usawa wa bahari na longitudo na E, Sura ya nchi, longitudo na latitudo.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayoathiri tabianchi ya eneo fulani katika uso wa dunia. Kwani majibu hayo yalichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, Gridi ni mistari ya ulalo na wima inayochorwa katika ramani na inayotumiwa kutambua maeneo kwenye ramani. Meridiani Kuu ni mstari wa kudhaniwa kwenye uso wa dunia kutoka ncha ya Kaskazini hadi ncha ya Kusini ya dunia hutumika kuonesha utofauti wa tarehe. Sura ya nchi huundwa na maumbo ya aina mbalimbali kama vile milima, tambarare, mabonde na maji yanayopatikana juu ya ardhi. Mstarihi ni mstari wa kudhaniwa wa tarehe wa kimataifa kwenye uso wa dunia kutoka ncha ya Kaskazini hadi ncha ya Kusini na hutumika kama mpaka kati ya siku moja ya kalenda na inayofuata. Longitudo ni mistari ya kufikirika inayoanzia ncha ya Kaskazini hadi ncha ya Kusini ambayo huchorwa magharibi na mashariki mwa meridian kuu. Mistari hii hutumika kupima ongezeko la umbali kutoka usawa wa bahari. Hivyo, machaguzi yaliyohusisha hoja hizi yanakuwa si sahihi.

**Swali la 26:** Ni kwa namna gani Tanzania inaweza kudumisha utamaduni wake?

- A Kwa kukusanya na kutunza vitu vya kisasa vya tamaduni za Ulaya
- B Kwa kuanzisha na kuendeleza vituo vya urithi wa utamaduni
- C Kwa kuazima mila na desturi kutoka katika tamaduni za kisasa za Ulaya
- D Kwa kutunza vituo vya urithi na utamaduni vya tamaduni za kigeni
- E Kwa kuzuia wageni kuja nchini mwetu

**Jedwali Na. 26: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	148,622	751,353	147,564	178,542	115,599	14,621
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	10.96	55.40	10.88	13.16	8.52	1.08

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha jinsi Tanzania inavyoweza kudumisha utamaduni wake. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 751,353 (55.40%) walichagua jibu sahihi *B*, *Kwa kuanzisha na kuendeleza vituo vya urithi wa utamaduni*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utunzaji wa utamaduni wa Mtanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 474,728 (35.00%) waliochagua vipotoshi; *A*, *Kwa kukusanya na kutunza vitu vya kisasa vya utamaduni wa Ulaya*, *C*, *Kwa kuazima mila na desturi kutoka katika tamaduni za kisasa za Ulaya* na *D*, *Kwa kutunza vituo vya urithi na utamaduni vya tamaduni za kigeni*, hawakuwa na uelewa juu ya utunzaji wa utamaduni wa Kitanzania. Vipotoshi hivyo vinaelezea zaidi juu ya utunzaji wa utamaduni wa kigeni. Vilevile, watahiniwa 115,599 (8.52%) waliochagua kipotoshi *E*, *Kuzuia wageni kuja nchini mwetu*, hawakuwa na uelewa kuwa, kitendo hicho kitasababisha nchi kukosa fedha za kigeni. Zaidi ya hapo kuwazuia wageni kuja nchini kunaweza kusababisha nchi kutengwa katika jumuiya ya kimataifa. Watahiniwa hawa walipaswa kutambua kuwa vitendo hivi havichangii kutunza utamaduni wa Mtanzania.

**Swali la 27:** Jambo lipi kati ya yafuatayo **si** miongoni mwa mafunzo wanayopatiwa vijana wakati wa sherehe za Jando na Unyago?

- A Kuheshimu wakubwa tu
- B Upendo kwa wanajamii
- C Kujitegemea
- D Kupenda kazi
- E Malezi ya vijana wakati wa balehe

**Jedwali Na. 27: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	708,152	152,440	185,079	93,012	201,474	16,144
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	52.21	11.24	13.65	6.86	14.85	1.19

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini jambo ambalo si mafundisho ya Jando na Unyago kwa vijana. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 708,152 (52.21%) walichagua jibu sahihi *A, Kuwaheshimu wakubwa tu*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utunzaji wa mila za Kitanzania. Walitambua kuwa wakati wa Jando na Unyango vijana hufundishwa nyanja mbalimbali za maisha kama vile kuwaheshimu watu wote katika jamii na sio kuwaheshimu wakubwa tu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 632,005 (46.60%) waliochagua vipotoshi *B, Upendo kwa wanajamii, C, Kujitegemea, D, Kupenda kazi* na *E, Malezi ya vijana wakati wa balehe*, walitoa majibu yasiyo sahihi, kwa sababu, vipotoshi viliundwa na mafundisho yatolewayo kwa vijana wakati wa sherehe za Jando na Unyago.

**Swali la 28:** Ni vifaa gani hutumika katika ngoma za asili?

- A Zumari, marimba na piano
- B Zumari, piano na gitaa
- C Marimba, ngoma na zeze
- D Marimba, piano na gitaa la solo
- E Piano, zeze na ngoma

**Jedwali Na. 28: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	99,839	68,274	1,012,909	62,166	102,113	11,000
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	7.36	5.03	74.68	4.58	7.53	0.82

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha vifaa vinavyotumika katika ngoma za asili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 1,012,909 (74.68%) walichagua jibu sahihi C, *Marimba, ngoma na zeze*. Uchaguzi wa jibu hili unadhihirisha uelewa wa kutosha juu ya vifaa vinavyotumika katika ngoma za asili ambazo hutunza utamaduni wa Mtanzania.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 332,392 (24.51%) walichagua vipotoshi; A, *Zumari, marimba na piano*, B, *Zumari, piano na gitaa*, D, *Marimba, piano na gitaa la solo* na E, *Piano, zeze na ngoma*. Majibu hayo hayakuwa sahihi, kwa sababu, yalikusisha vifaa kama vile piano, gitaa na gitaa la solo ambavyo ni vifaa vya kisasa vinavyotumika katika ngoma za ugaibuni.

**Swali la 29:** Elimu ya jadi ya Afrika ilifundisha stadi kadhaa kama vile usafi binafsi, kujitegemea, utunzaji wa mazingira na kuheshimu watu wengine. Elimu hiyo inaweza kutathminiwa vipi?

- A Ilitoa stadi za maarifa yenye uhalisia
- B Ilifaa kuigwa na wageni kutoka nje ya Afrika
- C Ilikuwa ya kukariri kwa vile wanafunzi hawakuandika nukuu
- D Ilizuia kupata elimu ya kigeni
- E Ilitolewa kwa matabaka

**Jedwali Na. 29: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	750,344	223,923	145,418	111,909	110,833	13,874
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	55.32	16.51	10.72	8.25	8.17	1.02

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini namna elimu ya jadi ya Kiafrika inavyoweza kutathiminiwa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 750,344 (55.32%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Ilitoa stadi za maarifa yenye uhalisia*. Watahiniwa waliochagua jibu hili walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maudhui

ya elimu ya jadi. Walielewa kuwa elimu ya jadi iliwafundisha vitu ambavyo vinawawezesha kuishi vyema katika mazingira yao hivyo kuweza kuchagua jibu sahihi.

Kinyume na hapo, watahiniwa 592,085 (43.62%) walichagua vipotoshi; *B, Ilifaa kuigwa na wageni kutoka nje ya Afrika, C, Ilikuwa ya kukariri kwa vile wanafunzi hawakuandika nukuu, D, Ilizuia kupata elimu ya kigeni na E, Ilitolewa kwa matabaka*. Kipotoshi B kuhusu kuigwa na wageni, si kila jambo linaloigwa ni zuri hivyo siyo jibu sahihi. Kuhusu kukariri katika kipotoshi C, elimu hii iliotelewa kwa vitendo hivyo si kwa kukariri kwani mwanafunzi alishiriki katika ujifunzaji. Aidha, kuandika nukuu tu hakumfanyi mwanafunzi kuelewa anachojifunza. Elimu ya jadi haikuzuia wageni kujifunza bali ilifundisha kila mtu aliyeishi katika jamii husika. Katika kipotoshi E kuhusu kutolewa kulingana na matabaka, elimu ya jadi haikuzingatia matabaka bali ilitolewa kwa kuzingatia umri na jinsia.

**Swali la 30:** Baadhi ya mataifa ya kibepari yaligawana Afrika Mashariki kwa njia ya makubaliano au mikataba. Waingereza walipewa utawala wa Uganda kwa mkataba upi?

- A Mkataba wa Berlin wa mwaka 1884 hadi 1885
- B Mkataba wa Heligoland wa mwaka 1890
- C Mkataba wa Waingereza na Wajerumani wa mwaka 1886
- D Mkataba wa Heligoland wa mwaka 1886
- E Mkataba wa Waingereza na Wajerumani wa mwaka 1885

**Jedwali Na. 30: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	502,671	340,800	188,252	181,806	123,799	18,973
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	37.06	25.13	13.88	13.40	9.13	1.40

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini mkataba ambao uliwapa Waingereza haki ya kuitawala Uganda. Ufaulu wa watahiniwa katika

swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 996,528 (73.47%) walichagua majibu yasiyo sahihi. Watahiniwa 502,671 (37.06%) waliochagua kipotoshi A, *Mkataba wa Berlin wa mwaka 1884 hadi 1885*, hawakuelewa kuwa, Mkutano wa Berlin ulilenga kuligawa bara la Afrika kwa mataifa ya kibepari kwa njia ya amani. Watahiniwa wengine 188,252 (13.88%) walichagua kipotoshi C, *Mkataba wa Waingereza na Wajerumani wa mwaka 1886*. Katika mkataba huu Wajerumani na Waingereza walitambua eneo la utawala la Sultani ambalo ni Zanzibar, Pemba, Lamu, Mogadishu, Maca, Brava na maili 10 za ukanda wa pwani wa Bahari ya Hindi. Watahiniwa 181,806 (13.40%) waliochagua kipotoshi D, *Mkataba wa Heligoland wa mwaka 1886*, hawakutambua kuwa, mkataba huo haukuwepo. Vilevile, watahiniwa 123,799 (9.13%) waliochagua kipotoshi E, *Mkataba wa Waingereza na Wajerumani wa mwaka 1885*, hawakuelewa kuwa, Waingereza na Wajerumani hawakufanya mkataba mwaka 1885. Hiki ni kipindi ambacho ndugu Karl Peters aliwasilisha mkataba kwa Kansela Otto von Bismarck na Rais Kaiser William I. Mkataba huo ulieleza kuwa maeneo yote aliyoyatembelea yaliwekwa kuwa makoloni ya Ujerumani.

Hata hivyo watahiniwa 340,800 (25.13%) waliochagua jibu sahihi B, *Mkataba wa Heligoland wa mwaka 1890*, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mikataba mbalimbali iliyofanywa na mabepari kuigawa Afrika Mashariki. Hivyo, waliweza kubainisha mkataba uliowafanya Waingereza kuitawala Uganda.

**Swali la 31:** Zifuatazo ni athari anazoweza kuzipata mtoto wa kike aliyeketwa **isipokuwa:**

- A kukwama kwa utendaji kazi wa asili wa mwanamke.
- B kuharibika kwa viungo vya uzazi vya mwanamke.
- C kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua.
- D kupata matatizo wakati wa kujifungua.
- E kupata magonjwa yasiyoambukiza.



**Jedwali Na. 31: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	426,804	114,440	130,146	70,350	59,8417	16,144
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	31.47	8.44	9.60	5.19	44.12	1.18

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha athari isiyoweza kumpata mtoto wa kike aliyekeketwa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 598,417 (44.12%) walichagua jibu sahihi *E, kupata magonjwa yasiyoambukiza*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya athari zinazotokana na ukeketaji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 741,740 (54.69%) walichagua vipotoshi; *A, kukwama kwa utendaji kazi wa asili wa mwanamke, B, kuharibika kwa viungo vya uzazi vya mwanamke, C, kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua na D, kupata matatizo wakati wa kujifungua*. Watahiniwa hao walitakiwa kutambua kuwa haya ni madhara ya ukeketaji. Hivyo, walikuwa kinyume na matakwa ya swali.

**Swali la 32:** Mwalimu alimuuliza Amina ataje chombo kinachopitisha bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Amina alitaja chombo kipi?

- A Sekretarieti ya Jumuiya    B Mkutano Maalum  
 C Mkutano Mkuu                      D Baraza la Mawaziri  
 E Bunge la Jumuiya

**Jedwali Na. 32: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	269,654	89,664	165,166	223,126	59,1464	17,227
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	19.88	6.61	12.18	16.45	43.61	1.27

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua chombo kinachopitisha bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 591,464 (43.61%) walichagua jibu sahihi *E, Bunge la Jumuiya*. Uchaguzi wa jibu hili sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya majukumu mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo waliweza kubaini chombo kinachopitisha bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kinyume na hapo, watahiniwa 269,654 (19.88%) walichagua kipotoshi *A, Sekretarieti ya Jumuiya*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa, hiki ni chombo kinachoshughulika na shughuli za kila siku za Jumuiya. Watahiniwa 89,664 (6.61%) waliochagua kipotoshi *B, Mkutano Maalum*, walishindwa kutambua kuwa, huu ni mkutano wa Wakuu (Marais) wa Nchi wanachama kwa dhumuni la kupanga mipango na dira juu ya utambuzi wa malengo na madhumuni ya jumuiya. Vilevile, watahiniwa 165,166 (12.18%) waliochagua kipotoshi *C, Mkutano Mkuu*, hawakuelewa kuwa, kazi ya mkutano mkuu ni kutunga sera na kuratibu shughuli za jumuiya. Kwa kawaida, mkutano mkuu huitishwa mara moja kwa mwaka. Pia, mwenyekiti wa jumuiya huchaguliwa na mkutano huo. Watahiniwa wengine 223,126 (16.45%) waliochagua kipotoshi *D, Baraza la Mawaziri*, hawakufahamu kuwa, Baraza halipitishi bajeti bali huandaa mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama na huunganisha Mkutano Mkuu na shughuli za kila siku za jumuiya.

**Swali la 33:** Nani aliongoza Waafrika huko Kilwa Kivinje kupinga Wajerumani mwaka 1890?

- A Abushiri bin Sultani      B Hassan bin Makunganya
- C Mtemi Mchemba          D Kinjeketile Ngwale
- E Bwana Heri

### Jedwali Na. 33: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	256,426	233,328	196,482	483,252	168,506	18,307
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	18.91	17.20	14.49	35.63	12.42	1.35

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua kiongozi aliyewaongoza Waafrika kuwapinga Wajerumani maeneo ya Kilwa Kivinje mwaka 1890. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,104,666 (81.45%) walichagua vipotoshi; A, C, D and E. Watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutambua viongozi waliopinga utawala wa Wajerumani. Watahiniwa 10,437 (77%) waliochagua kipotoshi A, *Abushiri bin Sultani*, hawakuwa na uelewa kuwa Abushiri alipinga uvamizi wa Wajerumani katika ukanda wa Pwani, hususani maeneo ya Pangani mkoani Tanga. Watahiniwa wengine 196,482 (14.49%) waliochagua kipotoshi C, *Mtemi Mchemba*, hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kiongozi aliyewaongoza Wayao kuwapinga Wajerumani mwaka 1890. Vilevile, watahiniwa 483,252 (35.63%) waliochagua kipotoshi D, *Kinjekitile Ngwale*, hawakutambua kuwa huyu hakuwa mtemi bali aliweza kuwajengea Imani ya ujasiri wananchi kuwa maji aliyowapa huzuia risasi zisiwadhuru wakati wa mapambano dhidi ya Wajerumani mwaka 1905 hadi 1907. Vita hii ilihusisha eneo kubwa la Kusini mwa Tanganyika kuanzia Kilosa hadi Dar es Salaam. Watahiniwa wengine 168,506 (12.42%) waliochagua kipotoshi E, *Bwana Heri*, hawakubaini matakwa ya swali, kwa sababu, Bwana Heri alikuwa kiongozi wa Wazigua katika ukanda wa Pwani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 233,328 (17.20%) walichagua jibu sahihi B, *Hassan bin Makunganya*. Uchaguzi huu unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa watawala wa Kiafrika, maeneo yao na mchango walioutoa katika jamii zao. Hivyo, waliweza kubaini kiongozi aliyewapinga Wajerumani maeneo ya Kilwa Kivinje mwaka 1890.

- Swali la 34:** Kwa nini Mwalimu Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah wanatambulika kama mashujaa?
- A Walihamasisha watu kutengana wakati wa kudai uhuru
  - B Walipendekeza na kusimamia mbinu za kudai uhuru
  - C Hawakutumia mali binafsi kudai uhuru
  - D Hawakusafiri kwenda nchi za nje wakati wa kudai uhuru
  - E Waliongoza vyama vingi vya siasa katika nchi zao

**Jedwali Na.34: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	127,546	769,269	111,357	80,843	252,315	14,971
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	9.40	56.72	8.21	5.96	18.60	1.11

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua sababu inayowatambulisha Mwalimu Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah kama mashujaa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 769,269 (56.72%) walichagua jibu sahihi *B, Walipendekeza na kusimamia mbinu za kudai uhuru*. Watahiniwa hao walidhihirisha uelewa wa kutosha kuhusu kuwaenzi mashujaa wetu waliotoa mchango muhimu katika kudai uhuru wa nchi za Afrika.

Hata hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi; A, C, D na E walionesha ukosefu wa maarifa ya sifa zinazomfanya mtu kuwa shujaa. Kwa mfano; watahiniwa 127,546 (9.40%) waliochagua kipotoshi A, *Walihamasisha watu kutengana wakati wa kudai uhuru*, hawakuwa na uelewa kuwa Mwl Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah ni viongozi waliohamasisha zaidi umoja na mshikamano kwa Waafrika. Watahiniwa wengine 111,357 (8.21%) waliochagua kipotoshi C, *Hawakutumia mali binafsi kudai uhuru*, hawakutambua kuwa Mwl Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah walikuwa ni wazalendo wa kweli waliojitoa maisha yao na mali zao kwa maslahi mapama ya umma wa nchi zao.

Vilevile, watahiniwa 80,843 (5.96%) waliochagua kipotoshi *D, Hawakusafiri kwenda nchi za nje wakati wa kudai uhuru*, hawakuwa na uelewa kuwa Mwl Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah walisafiri kwenda nchi za nje kwa lengo la kuhudhuria mkutano mbalimbali ili kupigania uhuru wa nchi zao. Kwa mfano Mwl Nyerere alienda katika mkutano wa Umoja wa Mataifa mwezi machi 1955 kudai uhuru wa Tanganyika. Pia, Kwame Nkurumah alihudhuria mkutano wa Wapigania Uhuru wa Afrika mwaka 1945 katika jiji la Manchester nchini Uingereza. Watahiniwa wengine 252,315 (18.60%) walichagua kipotoshi *E, Waliongoza vyama vingi vya siasa katika nchi zao*. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, Mwl Julius K. Nyerere alikuwa kiongozi wa chama cha TANU kuanzia mwaka 1954 hadi 1977. Baadae TANU kiliungana na ASP kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kwame Nkurumah alikuwa kiongozi wa chama cha CPP kuanzia mwaka 1949 hadi 1966. Hivyo, mashujaa hawa waliongoza chama kimoja cha siasa na si vyama vingi katika nchi zao.

**Swali la 35:** Wakati wa uvamizi wa kikoloni, baadhi ya mashujaa hawakuwa tayari kukamatwa na wakoloni. Yupi alijiua ili kukwepa kukamatwa na wakoloni?

- A Chifu Mkwawa                      B Chifu Mirambo  
C Chifu Merere                        D Chifu Isike  
E Chifu Makunganya

**Jedwali Na. 35: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	801,606	173,676	108,644	163,735	93,331	15,309
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	59.10	12.81	8.01	12.07	6.88	1.13

Swali lilimtaka mtahiniwa kumbaini shujaa wa Afrika aliyejiua ili kukwepa kukamatwa na wakoloni. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 801,606 (59.10%) waliochagua jibu sahihi A, *Chifu Mkwawa*, walionesha uelewa wa kutosha. Waliweza kubaini kuwa, Chifu Mkwawa alijipiga risasi

mwenyewe tarehe 09 Julai 1898 mkoani Iringa ili kuepuka kukamatwa na Wajerumani.

Vilevile, watahiniwa waliochagua vipotoshi; B, C, D na E, walionesha kutokuwa na maarifa juu ya mchango wa viongozi mbalimbali waliopinga uvamizi wa wakoloni. Kwa mfano; Watahiniwa 173,676 (12.8%) waliochagua kipotoshi *B, Chifu Mirambo*, walikosa ufahamu kuwa, Mirambo alikuwa Mtemi imara wa Unyanyembe mkoani Tabora aliyewaunganisha Wanyamwezi na kuwa himaya imara katika miaka ya 1870, alikufa mwaka 1884. Watahiniwa wengine 108,644 (8.01%) waliochagua kipotoshi *C, Chifu Merere*, hawakutambua kuwa Merere alikuwa Mtemi wa Wasangu wa Mbarali mkoani Mbeya ambaye alikamatwa na kuuawa na Wajerumani mwaka 1893. Vilevile, watahiniwa 163,735 (12.07%) waliochagua kipotoshi *D, Chifu Isike*, walikosa maarifa kuwa, Isike alikuwa kiongozi wa Wanyamwezi katika Unyanyembe mkoani Tabora aliyetawala kuanzia mwaka 1885 na kufa mwaka 1893. Vivyo hivyo, watahiniwa 93,331 (6.88%) walichagua kipotoshi *E, Chifu Makunganya*. Hawakuwa na uelewa kuwa, Mtemi Makunganya aliwaongoza waafrika kuwapinga Wajerumani katika maeneo ya Kilwa Kivinje mwaka 1890. Alikufa tarehe 26 Novemba 1895 baada ya kukamatwa na kuuawa na Wajerumani.

**Swali la 36:** Kwa nini ni muhimu kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula?

- A Ili kuwafurahisha wazazi
- B Ili kujikinga na magonjwa
- C Ili kuonyesha usasa
- D Ili kutekeleza utaratibu
- E Ili kuiga utamaduni wa kigeni

**Jedwali Na. 36: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	52,694	1,167,039	50,272	44,383	30,422	11,491
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	3.89	86.05	3.71	3.27	2.24	0.84

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini umuhimu wa kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 1,167,039 (86.05%) walichagua jibu sahihi *B, Ili kujikinga na magonjwa*. Uchaguzi wa jibu hili unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu usafi binafsi na hasa umuhimu wa kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 177,771 (13.11%) walichagua vipotoshi *A, Ili kuwafurahisha wazazi, C, Ili kuonyesha usasa, D, Ili kutekeleza utaratibu na E, Ili kuiga utamaduni wa kigeni*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu usafi binafsi na hasa umuhimu wa kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula. Kwa mfano watahiniwa 52,694 (3.89%) waliochagua kipotoshi *A, Ili kuwafurahisha wazazi* waliamini kuwa ni jukumu la wazazi kuwafundisha na kuwajengea watoto wao tabia ya kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula. Vilevile, watahiniwa 50,272 (3.71%) waliochagua kipotoshi *C, ili kuonyesha usasa* waliamini kuwa kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula ni tendo la ustaarabu kote duniani. Watahiniwa wengine 44,383 (3.27%) waliochagua kipotoshi *D, Ili kutekeleza utaratibu* walihusianisha na mazoea ya kila siku kwa vile imekuwa ni kawaida na desturi au tabia ya kila wakati wa kula kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula. Vivyo hivyo, watahiniwa 30,422 (2.24%) waliochagua kipotoshi *E, Ili kuiga utamaduni wa kigeni* waliamini kuwa kunawa mikono kwa sabuni siyo utamaduni wao bali ni wa kuiga kutoka kwa wageni.

**Swali la 37 :** Je, Litungu na Zeze zipo katika kundi lipi la ala za muziki?

- A Kupuliza      B Kugonga      C Kukwaruza
- D Kubonyeza    E Kutikisa

**Jedwali Na. 37: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	288,564	175,534	638,634	108,446	128,281	16,842
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	21.28	12.94	47.09	8.00	9.46	1.24

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubaini kundi la ala ambalo Litungi na Zeze zinapatikana. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 638,634 (47.09%) walichagua jibu sahihi C, *Kukwaruza*. Uchaguzi wa jibu sahihi unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa ala mbalimbali za muziki na namna zinavyofanya kazi za kuzalisha sauti hivyo kuweza kubaini kuwa Litungu na Zeze ni ala za muziki zinazozalisha sauti kwa kukwaruza.

Watahiniwa wengine 700,825 (51.67%) waliochagua vipotoshi A, *Kupuliza*, B, *Kugonga*, D, *Kubonyeza* na E, *Kutikisa*, walishindwa kutambua ala mbalimbali za muziki na jinsi zinavyotumika kuzalisha sauti. Ala kama filimbi na baragumu ndiyo hutoa sauti kwa kupuliza. Ngoma na marimba hutoa sauti kwa kugonga, kinanda na gitaa la mkono hutoa sauti kwa kubonyeza na manyanga ni mfano wa ala ambayo hutoa sauti kwa kutikisa.

**Swali la 38:** Wanafunzi wa Darasa la Tano walijifunza namna ya kufanya usafi katika sakafu za aina tofauti. Je, ni aina ipi ya sakafu walijifunza kunyunyizia maji kabla ya kufagia?

- A Mbao                      B Udongo                      C Saruji  
D Tarazo                      E Marumaruru



### Jedwali Na.38: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	55,625	788,657	223,670	93,176	178,239	16,934
Asilimia ya Watahiniwa	4.10	58.15	16.49	6.87	13.14	1.25

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuainisha sakafu ambayo hutakiwa kunyunyizia maji kabla ya kufagia. Ufaulu wa jumla ulikuwa wa wastani kwasababu watahiniwa 788,657 (68.15%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Udongo*. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kufanya usafi katika sakafu za aina tofauti tofauti. Hivyo, waliweza kubaini kuwa sakafu ya udongo huitaji kunyunyiziwa maji kabla ya kufagia, ili kuzuia vumbi ambalo lingeweza kutimuka endapo sakafu ingefagiliwa bila kunyunyiziwa maji.

Tofauti na hivyo, jumla ya watahiniwa 550,710 (40.60%) walichagua vipotoshi; *A, Mbao, C, Saruji, D, Tarazo* na *E, Marumaru*. Uchaguzi wa majibu hayo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kufanya usafi katika sakafu za aina tofauti tofauti kwani hizi ni sakafu za kisasa ambazo hazihitaji kunyunyiziwa maji kwa vile hazizalishi vumbi watu wanapotembea juu yake. Sakafu ya Saruji, Tarazo na Marumaru husafishwa kwa kumwaga maji safi na sabuni kiasi, kisha husuguliwa kwa kutumia brashi na hukaushwa kwa kutumia dekio safi. Wakati sakafu za mbao hazihitaji kabisa kumwagiwa maji mengi bali husafishwa kwa kufagia na kufutwa kwa kutumia kitambaa kilichokamuliwa maji.

**Swali la 39 :** Ipi ni dalili ya balehe ambayo hujitokeza kwa wasichana na wavulana?

- A Sauti nzito
- B Kuota matiti
- C Kuwa na mihemko mbalimbali
- D Kuota ndoto nyevu
- E Kupata hedhi

**Jedwali Na. 39: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
<b>Idadi ya Watahiniwa</b>	109,175	75,833	748,261	293,800	113,530	15,702
<b>Asilimia ya Watahiniwa</b>	8.05	5.59	55.17	21.66	8.37	1.16

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha dalili ya balehe ambayo hujitokeza kwa wasichana na wavulana. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 748,261 (55.17%) walichagua jibu sahihi *C, Kuwa na mihemko mbalimbali*. Uchaguzi wa jibu hili unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dalili za balehe kwa wasichana na wavulana.

Hata hivyo, watahiniwa 592,338 (43.67%) walichagua vipotoshi *A, Sauti nzito, B, Kuota matiti, D, Kuota ndoto nyevu na E, Kupata hedhi*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dalili za balehe kwa wasichana na wavulana. Kwa mfano, sauti nzito na kuota ndoto nyevu ni dalili za balehe kwa wavulana. Kuota matiti na kupata hedhi ni dalili za balehe kwa wasichana.

**Swali la 40:** Bahati huuza chai ya maziwa na nyama choma kwa vibarua wa shamba la mkonge na hupata wateja wachache lakini Nyemo huuza chai ya rangi na mihogo kwa vibarua haohao na hupata wateja wengi sana. Kwa nini Bahati hupata wateja wachache?

- A Hazingatii kipato cha wateja
- B Anauza chakula kisichopendwa na wateja
- C Siyo mvumilivu kwa wateja
- D Hawaburudishi wateja
- E Hajui kupika vizuri

## Jedwali Na. 40: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	363,982	495,969	238,462	142,803	99,125	15,960
Asilimia ya Watahiniwa	26.84	36.57	17.58	10.53	7.31	1.17

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu ya Bahati kupata wateja wachache. Ufaulu wa swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 976,359 (71.99%) walichagua vipotoshi B, Anauza chakula kisichopendwa na wateja, C, *Siyo mvumilivu kwa wateja, D, Hawaburudishi wateja* na E, *Hajui kupika vizuri*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuweza kubainisha namna mbalimbali ambazo mjasiriamali anaweza kuzitumia ili kuwavutia wateja na kuwahudumia kwa kadri ya mahitaji yao.


Kwa upande mwingine watahiniwa 363,982 (26.84%) walichagua jibu sahihi A, *Hazingatii kipato cha wateja*. Uchaguzi wa jibu hili unaonesha kuwa, watahiniwa hao waliweza kubainisha namna mbalimbali ambazo mjasiriamali anaweza kuzitumia ili kuwavutia wateja na kuwahudumia kwa kadri ya mahitaji yao. Aidha, waliweza kutambua mambo ya kuzingatia katika kutafuta masoko hususan kufanya uchunguzi wa kina kuhusu wateja au wanunuzi ili kuchagua bidhaa sahihi na bei watakayoimudu.

### 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

**Swali la 41:** Chama cha *Tanganyika African National Union* (TANU) kiliundwa mwaka 1954. Lipi lilikuwa lengo kuu la kuundwa kwake?

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza lengo kuu la kuundwa kwa Chama cha *Tanganyika African National Union* (TANU) mwaka 1954. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani, watahiniwa 735,816 (54.25%) walipata alama 01 na 02 na watahiniwa 620,485

(45.75%) walipata 00. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41.



**Chati Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 41

Jumla ya watahiniwa 720,355 (53.11%) walipata alama 02, kwa sababu, walitaja kwa usahihi lengo kuu la kuundwa kwa chama hicho ambalo ni kuwaunganisha wananchi wa Tanganyika katika kupigania Uhuru wao. Usahihi wa jibu hili unathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mbinu zilizotumika katika harakati za kudai Uhuru katika Tanganyika. Chama cha Tanganyika African National Union (TANU) kiliundwa kutokana na kukithiri kwa unyonyaji, hasa baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Kielelezo Na: 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa mwenye maarifa ya kutosha katika swali hili.

<b>SWALI LA 41</b>
<i>lli kupigania uhuru wa Tanganyika</i>

**Kielelezo Na 1.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 41

Kwa upande mwingine, watahiniwa 620,485 (45.75%) waliopata sifuri, walikuwa na udhaifu mbalimbali katika majibu yao. Kwa mfano mtahiniwa mmoja katika kundi hili aliandika “kuunga mkono vyama vya siasa”. Mtahiniwa huyo alishindwa kuelewa lengo kuu la TANU ambalo lilikuwa kuwaunganisha Watanganyika kudai uhuru wao na sio kuunga mkono vyama vya siasa. Pia, mtahiniwa mwingine katika kundi hili aliandika “kuimarisha TAA” jambo linaloashiria hakuwa na uelewa kuwa, chama cha Tanganyika African Association (TAA) kiliundwa mwaka 1929. Kwa hiyo, ili kukiimarisha, kilibadilishwa na kuwa, Tanganyika National Union (TANU) mwaka 1954, hivyo, ilikuwa ni chama cha TANU na sio TAA kilichowaunganisha Watanganyika kudai uhuru mwaka 1961. Vilevile, mtahiniwa mwingine alijibu, “ili kuleta sera ya ujamaa na kujitegemea”. Mtahiniwa huyu hakuelewa kuwa, sera ya ujamaa na kujitegemea ilitambulishwa na Mwl. Julius K. Nyerere wakati wa Azimio la Arusha mwaka 1967. Hivyo ilidhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu lengo la TANU. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


SWALI LA 41
Mfumo wa vyama vingi

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 41

Katika kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa aliandika mfumo wa vyama vingi badala ya lengo kuu la kuundwa kwa Chama cha Tanganyika African National Union (TANU) mwaka 1954.

**Swali la 42:** Mzee Maina anamiliki ng’ombe 2,800 na huhama kutoka eneo moja kwenda jingine. Mwaka jana alikuwa Singida, mwezi uliopita alikuwa Dodoma na kwa sasa yupo Morogoro. Toa sababu mbili zinazomfanya Mzee Maina kuhamahama.

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa sababu za Mzee Maina kufanya ufugaji wa kuhamahama. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani, watahiniwa 884,107 (65.19%) walipata alama 01 na 02, na watahiniwa 472,194 (34.81%) walipata 0. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 42.



**Chati Na. 2:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 42

Katika swali hili, jumla ya watahiniwa 376,074 (27.73%) walipata alama 02 kwani waliandika sababu mbili kwa usahihi. Sababu walizotoa ni pamoja na ukosefu wa malisho na ukosefu wa maji. Usahihi wa majibu hayo unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sababu za ufugaji wa kuhamahama ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na ukosefu wa chakula na maji mambo yanayochangiwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa.

SWALI LA 42	
(i)	Uhaba wa maji.
(ii)	Uhaba wa chakula.

**Kielelezo Na 2.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 42

Vivyo hivyo, watahiniwa 508,03 (37.46%) walipata alama 01, kwa sababu walitoa jibu sahihi na lisilo sahihi. Majibu hayo yanathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu aina za ufugaji unaofanyika Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa ufugaji wa kuhamahama hufanywa na watu wenye mifugo mingi ambao hawawezi kupata majani na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo katika eneo moja. Hali ya kukosa chakula na maji husababisha mifugo kufa. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika majibu ambayo ni *kutafuta malisho na soko la ng'ombe* ambapo hoja ya kutafuta soko la ng'ombe si sahihi hivyo alipata alama 01.

Tofauti na hivyo, watahiniwa 472,194 (34.81%) walipata alama 0. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu sababu za ufugaji wa kuhamahama, kwani walitoa majibu tofauti na matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa walihusianisha madhara yatokanayo na ufugaji wa wanyama wengi katika eneo dogo ambapo humaliza nyasi zote na uoto na kuacha ardhi tupu, pia hufanya ardhi kuwa tifutifu na kusababisha upepo na mvua kuimomonyoa kwa urahisi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika ufugaji wa kuhamahama husababisha ukataji miti ovyo ili kutengeneza mazizi, makazi na kupata kuni za kupikia. Mtahiniwa mwingine aliandika *Mzee huyo anahama ili kuepuka kusababisha mmomonyoko wa udongo*. Majibu hayo yalidhihirisha kukosa uelewa juu ya mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa.


SWALI LA 42
(i) ili: Kutunza mazingira
(ii) ili: Kuongeza rutuba

**Kielelezo Na 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 42

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa aliandika mbinu za kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na ufugaji usiofaa badala ya sababu za ufugaji wa kuhamahama.

**Swali la 43:** Wanafunzi walipima umbali katika ramani ya kijiji kutoka kwenye kisima cha maji hadi zahanati ikiwa umbali katika ramani ni kupata sentimeta 5. Tafuta umbali halisi ikiwa kipimio cha ramani ni 1: 300,000.

Swali lilimtaka mtahiniwa kutafuta umbali halisi kutoka kwenye kisima cha maji hadi zahanati ikiwa umbali katika ramani ni sentimeta 5 na kipimio cha ramani ni 1:300,000. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,271,156 (93.72%) walipata 0. Kwa upande mwingine, watahiniwa 12,314 (0.91%) walipata alama 01 na watahiniwa 72,831 (5.37%) walipata alama 02. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 43.



**Chati Na. 3:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 43

Watahiniwa 1,271,156 (93.72%) waliopata alama 0 hawakuweza kujibu swali kwa usahihi, kwa sababu baadhi yao walitumia kanuni isiyo sahihi kupata jibu kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu kanuni ya kutafuta umbali halisi katika ardhi kwa kutumia vipimio ambavyo hutolewa katika ramani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika  $300,000 \times 5 = 1,500,000$ . Katika swali hili watahiniwa wengi walikosa umahiri wa kuhusianisha vipimo kwani walishindwa kubadili sentimeta ili kupata kilometa. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa.



SWALI LA 43
1:300,000

**Kielelezo Na 3.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 43

Katika Kielelezo Na. 3.1 mtahiniwa alinakili kutoka kwenye swali kipimio cha ramani alichokuwa amepewa (1:300,000) badala ya kutafuta umbali halisi kutoka kwenye kisima hadi zahanati.

Zaidi ya hapo, watahiniwa 72,831 (5.37%) waliopata alama 02 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kanuni ya kutafuta umbali halisi katika ramani ikiwa umepewa kipimio cha ramani. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuhusianisha vipimo hivyo, kuweza kubadili sentimeta kuwa kilometa na kupata jibu sahihi ambalo ni kilometa 15. Baadhi ya watahiniwa walifuata hatua zifuatazo kikamilifu;

$$\begin{array}{l} 1 \text{ cm} = 3 \text{ km} \\ 5 \text{ cm} = M \end{array}$$

$$\frac{1 \text{ cm} \times M}{1 \text{ cm}} = \frac{5 \text{ cm} \times 3 \text{ km}}{1 \text{ cm}}$$

$$M = \frac{15 \text{ km}}{1}$$

$$M = 15 \text{ km}$$

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa.

SWALI LA 43


$$1 \text{ --- } 5\text{cm} = 5 \times 3$$

$$300000 \text{ --- } x = \text{Km } 15$$

**Kielelezo Na 3.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 43

**Swali la 44:** Usafirishaji ni moja ya shughuli muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Ni vitu gani viwili muhimu vinahitajika ili usafirishaji ufanyike kwa urahisi?

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutaja vitu viwili muhimu vinavyohitajika ili usafirishaji ufanyike kwa urahisi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani, watahiniwa 961,233 (70.87%) walipata alama 01 na 02. Kwa upande mwingine, watahiniwa wengine 395,068 (29.13%) walipata 0. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44.



**Chati Na. 4:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 44

Jumla ya watahiniwa 405,757 (29.92%) walipata alama 02 kwasababu walitaja kwa usahihi vitu viwili muhimu vinavyohitajika ili usafirishaji ufanyike kwa urahisi. Watahiniwa hao walitoa majibu kama; *uwepo wa watu, uwepo wa mizigo, mtaji na miundombinu.*

Usahihi wa majibu hayo unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya usafirishaji na hasa vitu vinavyofanya usafirishaji ufanyike kwa urahisi. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi katika swali la 44.

<b>SWALI LA 44</b>
Y WATU
Y BIDHAA (MAKIGHAFI)

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 44

Kwa upande mwingine, watahiniwa 555,476 (40.96%) walipata alama 01 katika swali hili kwani walitoa hoja moja sahihi na isiyo sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu dhana ya usafirishaji na hasa mambo yanayosababisha usafirishaji uwe rahisi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika hoja ambazo ni *bidhaa* na *usafiri wa ardhini*. Mtahiniwa hakuwa sahihi kwenye hoja ya pili ambapo alitaja aina mojawapo ya njia za usafirishaji.

Tofauti na hivyo, watahiniwa 395,068 (29.13%) walipata alama 0 kwa sababu hawakuwa na uelewa kuhusu dhana ya usafirishaji na hasa mambo yanayosababisha usafirishaji uwe rahisi. Baadhi ya watahiniwa walitaja *vyombo vya usafiri*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *boti* na *ndege*. Mtahiniwa huyu alishindwa kubaini kuwa boti ni chombo kinachotumiwa kusafiria kwenye maji na ndege ni chombo cha usafiri wa anga. Watahiniwa wengine, waliandika sababu kama vile *uwepo wa hali ya hewa nzuri*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kutokuwepo kwa mvua nyingi*. Alihusianisha madhara yanayotokana na mvua katika miundo mbinu kama vile barabara, reli na viwanja nya ndege. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


SWALI LA 44
(a) Usafiri wa maji
(b) Usafiri wa anga

**Kielelezo Na 4.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa aliandika njia za usafirishaji badala ya vitu vinavyohitajika ili usafirishaji ufanyike kwa urahisi. Alishindwa kubaini kuwa usafiri wa maji ni njia ya kusafirisha abiria na bidhaa kwa njia ya maji wakati usafiri wa anga ni njia ya kusafirisha abiria na bidhaa kwa njia ya anga.

- Swali la 45:** (a) Kifaa gani kinatumika kupima mwanga wa jua?  
(b) Taja kipimio kinachotumika kupima mwanga wa jua.

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kubaini kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutaja kipimio kinachotumika kupima mwanga wa jua. Ufaulu wa jumla ulikuwa hafifu kwa sababu watahiniwa 881,864 (65.02%) walipata 0. Kwa upande mwingine, watahiniwa 371,828 (27.41%) walipata alama 01 na watahiniwa 102,609 (7.57%) walipata alama 02. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45.



**Chati Na. 5:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 45

Watahiniwa 881,864 (65.02%) waliopata alama 0 katika swali hili, walitoa majibu yasiyo sahihi kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu mada husika. Watahiniwa wengi walichanganya vifaa na vizio vya ujazo vya vipengele vya hali ya hewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika asilimia katika vipengele (a) na (b). Alishindwa kubaini kuwa hiki ni kizio cha ujazo kinachowasilisha au kurekodi unyevuanga. Mtahiniwa mwingine katika kipengele (a) aliandika haigrometa na (b) aliandika kipima mwanga. Mtahiniwa huyu alishindwa kubaini kuwa haigrometa ni kifaa kinachopima unyevuanga na kipimamwanga kinatumika kupima mwanga wa jua na siyo kipimio cha mwanga wa jua. Hata hivyo, mtahiniwa mwingine katika kipengele (a) aliandika Zebaki na (b) milimita. Huyu pia, alishindwa kubaini kuwa zebaki ni kimiminika kinachotumiwa katika kipimajoto na milimita ni kizio cha ujazo kinachowasilisha au kurekodi kiwango cha mvua. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha majibu yasiyo sahihi katika swali la 45.

<b>SWALI LA 45</b>	(a) Anemometa
	(b) barometa

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 45

Katika kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa aliandika anemometa, badala ya Kipima mwanga wa jua/Kampbeli stok katika kipengele (a). Katika kipengele (b) aliandika barometa, badala ya saa. Alishindwa kubaini kuwa anemometa ni kifaa kinachopima kasi ya upepo na barometa hupima mgandamizo wa hewa.

Watahiniwa 371,828 (27.41%) walipata alama 01. Watainiwa hawa walitoa jibu sahihi na lisilo sahihi. Walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu hali ya hewa na hasa vipengele vya hali ya hewa, namna vinavyopimwa na vipimio vyake. Baadhi ya watahiniwa walitoa jibu sahihi katika kipengele (a) na lisilo sahihi kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika milibaa katika kipengele (b). Mtahiniwa huyo hakutambua kuwa hiki ni kizio cha ujazo kinachowasilisha au kurekodi mgandamizo wa hewa.

Zaidi ya hapo, watahiniwa 102,609 (7.57%) walipata alama 02. Watahiniwa hao walitoa majibu sahihi katika vipengele vyote. Kipengele (a) waliandika Kipima mwanga wa jua/Kampbeli stok na kipengele (b) waliandika Saa. Usahihi wa majibu hayo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu hali ya hewa na hasa vipengele vya hali ya hewa, namna vinavyopimwa pamoja na vipimio vyake. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

SWALI LA 45
a) Kampbell Stok
b) Saa

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yaliyo sahihi katika swali la 45

### **3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI**

Somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi lilikuwa na mahiri nane (08) zilizotahiniwa. Mahiri hizo ni; *kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali*, kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku, kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, kutambua misingi ya uzalendo katika jamii, kumudu mapishi mbalimbali, kusanifu kazi za sanaa, kutumia misingi ya unadhifu na kutumia stadi za ujasiriamali.

Ufaulu wa watahiniwa umekuwa katika kiwango tofauti kwa kila umahiri. Kiwango kizuri cha ufaulu kilikuwa katika umahiri wa kumudu mapishi mbalimbali (86.05%), mahiri nne (04) zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ambazo ni; Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii (47.97%), kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka (53.73%), Kusanifu kazi za sanaa (47.09%), na kutumia misingi ya unadhifu (56.66%). Aidha, mahiri tatu (03) zilikuwa katika kiwango hafifu cha ufaulu ambazo ni Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishajimali (39.10%), Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku (31.42%) na Kutumia stadi za ujasiriamali (26.84%).

### **4.0 HITIMISHO**

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihamu wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi 2023 umeonesha kuwa, watahiniwa 1,049,779 (77.40%) walifaulu kwa kupata daraja A – C ambao ni ufaulu mzuri. Ufaulu huo mzuri umechangiwa na umahiri waliokuwa nao katika dhana mbalimbali zilizotahiniwa. Aidha, watahiniwa 306,445 (22.60%) waliofeli walikosa maarifa ya kutosha katika umahiri uliotahiniwa Ufaulu ulikuwa mzuri katika umahiri mmoja, wastani katika mahiri nne na hafifu katika mahiri tatu. Matokeo hayo yanaonesha kuwa, juhudi zinahitajika zaidi ili ufaulu uongezeke. Ni matumaini kuwa taarifa hii itasaidia mamlaka husika kuchukua hatua stahiki.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mahiri zilizotahiniwa, yafuatayo yanapendekezwa:

- (a) Wanafunzi wafanye ziara za kimasomo ili kujifunza katika mazingira halisi kuhusu vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa na jinsi ya kuvitumia. Aidha, kutembelea maeneo mbalimbali ya kihistoria na maeneo yanayolimwa mazao ya biashara nchini. Hii itawawezesha wanafunzi kuwa na kumbukumbu ya kudumu katika umahiri wa Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayo mzunguka na kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali.
- (b) Walimu kutumia njia ya kazi mradi katika umahiri wa kusanifu kazi za sanaa na Kutumia misingi ya unadhifu kwa kufanya matendo mbalimbali ya ufundishaji na ujifunzaji kama uchoraji wa picha, ususi, uchongaji, ushonaji, ufinyanzi, utengenezaji wa maumbo mbalimbali na usafi wa mavazi na mazingira ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na kumbukumbu ya kudumu.
- (c) Kutumia michoro, ramani na picha mbalimbali kufafanua dhana tofauti wakati wa ufundishaji na ujifunzaji hususan katika umahiri wa kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku.
- (d) Wanafunzi wafanye matendo mbalimbali ya kihisabati kwa kufanya mazoezi mengi ili waweze kumudu mbinu mbalimbali za kutafuta tofauti ya muda baina ya miji, kutafuta tofauti ya jotoridi kwenye maeneo tofauti na mbinu mbalimbali za kubadili vipimo.
- (e) Wanafunzi washauriwe na kusesitiziwa kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.



## KIAMBATISHO

### ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI KWA MWAKA 2022 NA 2023

Na.	Umahiri	Mtihani wa 2022				Mtihani wa 2023					
		Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni		
		Namba ya swali	(%) ya Ufaulu			Namba ya swali	(%) ya Ufaulu				
1	Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali	1	60.2	54.7	Wastani	1	44.43	39.1	Hafifu		
		2	73.87			2	10.1				
		3	19.2			3	29.79				
		4	81.62			4	44.82				
		5	52.33			5	57.85				
		6	24.59			6	17.98				
		7	58.7			7	36.9				
		8	57.34			8	58.44				
		41	64.47			9	19.9				
2	Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku	24	74.3	53.8	Wastani	10	38.42	31.42	Hafifu		
		25	47.7			11	23.57				
		26	52			12	22.83				
		27	57.8			13	30.71				
		28	40.5			14	31.25				
		45	50.2			15	65.93			16	32.38
						43	6.28			17	18.47
						3	Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka			26	50.67
27	17.48			19	64.93						
28	57.49	20	46.23								
29	18.45	21	42.26								
30	28.85	22	64.75								
31	23.86										

Na.	Umahiri	Mtihani wa 2022				Mtihani wa 2023			
		Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	(%) ya Ufaulu			Namba ya swali	(%) ya Ufaulu		
		32	42.97			23	62.2		
		33	43.88			24	76.49		
		34	59.09			25	44.6		
		35	28.92			42	65.19		
		43	53.04			45	34.98		
		44	48.34						
4	Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii	14	27.94	47.49	Wastani	26	55.4	47.97	Wastani
		15	55.09			27	52.21		
		16	17			28	74.68		
		17	46.58			29	55.32		
		18	63.19			30	25.13		
		19	62.11			31	44.12		
		20	46.49			32	43.61		
		21	22.72			33	17.2		
		22	68.3			34	46.72		
		23	46.48			35	59.1		
		24	57.39						
		25	71.43			41	54.25		
		45	32.71						
5	Kumudu mapishi mbalimbali	38	83.02	83.02	Mzuri	36	86.05	86.05	Mzuri
6.	Kusanifu kazi za sanaa	39	74.59	74.59	Mzuri	37	47.09	47.09	Wastani
7	Kutumia misingi ya unadhifu	36	22	19.38	Hafifu	38	58.15	56.66	Wastani
						39	55.17		

Na.	Umahiri	Mtihani wa 2022				Mtihani wa 2023			
		Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	(%) ya Ufaulu			Namba ya swali	(%) ya Ufaulu		
8	Kutumia stadi za ujasiriamali	40	49.48	49.48	Wastani	40	26.84	26.84	Hafifu

